# HOTUBA YA WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI MHESHIMIWA PROF. JOYCE LAZARO NDALICHAKO (MB.) AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2016/17

**DODOMA** **MEI, 2016**



“Natambua juhudi kubwa zimefanyika katika upanuzi wa elimu ya awali, msingi, sekondari na vyuo vikuu. Serikali ya awamu ya tano, itajielekeza katika kuongeza ubora wa elimu inayotolewa ikiwa ni pamoja na kuongeza mkazo katika masomo ya sayansi.”

***Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wakati akifungua rasmi Bunge la 11, tarehe 22 Novemba 2015.***

# YALIYOMO


YALIYOMO........................................................................ i

VIFUPISHO ...................................................................... iii

1.0 UTANGULIZI ..................................................... 1

2.0 DIRA, DHIMA NA MAJUKUMU YA WIZARA YA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI ............................................................................ 4

DIRA NA DHIMA YA WIZARA .......................... 4

MAJUKUMU YA WIZARA .................................. 4

3.0 VIPAUMBELE VYA WIZARA YA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI ............. 6

4.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA 2015/16 ................................................ 8

5.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU KWA MWAKA 2015/16 NA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2016/17 .......................... 10

5.1 UTUNGAJI NA UTEKELEZAJI WA SERA YA ELIMU ................................................ 10

5.2 UPATIKANAJI WA FURSA ZA ELIMU NA MAFUNZO ........................................ 14

5.3 KUINUA UBORA WA ELIMU NA MAFUNZO ............................................... 16

5.4 TAFITI NA HUDUMA KWA JAMII ............ 36

5.5 SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UBUNIFU…. 40

5.6 URATIBU WA TAASISI NA WAKALA ........ 49

5.7 USIMAMIZI WA UTEKELEZAJI WA PROGRAMU NA MIRADI .......................... 67

6.0 SHUKRANI ........................................................ 83

7.0 MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2016/17… 86

VIAMBATISHO ........................................................ 88

## VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| **DAAD** | Deutscher Akademischer Austausch Dienst |
| **DfID** | Department for International Development |
| **EU** | European Union |
| **FDC** | Folk Development Colleges |
| **ICT** | Information and Communication Technology |
| **KKK** | Kusoma, Kuandika na Kuhesabu |
| **LANES** | Literacy and Numeracy Education Support |
| **MMES** | Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari |
| **NACTE** | National Council for Technical Education |
| **NECTA** | National Examination Council of Tanzania |
| **OR-TAMISEMI** | Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| **OVC** | Orphans and Vulnerable Children |
| **SIDA** | Swedish International Development Agency |
| **SLADS** | School of Library Archives and Documen- tation Studies |
| **STHEP** | Science, Technology and Higher Education Project |

| | |
|---|---|
| **SWASH** | Schools Water Sanitation and Hygiene |
| **TEHAMA** | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| **TET** | Taasisi ya Elimu Tanzania |
| **UDSM** | University of Dar es Salaam |
| **UNESCO** | United Nations Educational Scientific and Cultural Organization |
| **UNICEF** | United Nations Children's Fund |
| **VETA** | Vocational Education and Training Authority |
| **VVU** | Virusi Vya Ukimwi |

## 1.0 UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** kufuatia taarifa iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii ndani ya Bunge lako Tukufu, ambayo imechambua Bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi, naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Kazi za Wizara kwa mwaka 2015/16 na Mpango wa Utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka 2016/17. Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi kwa mwaka wa fedha 2016/17.

2. **Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee kabisa na kwa heshima kubwa napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa imani kubwa aliyoonesha kwangu kwa kuniteua kuwa Mbunge na Waziri wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi. Ninatambua ukubwa wa dhamana aliyonipa na changamoto zilizopo katika Sekta hii. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Rais na wananchi wote kwa ujumla kuwa nitafanya kazi hii kwa uadilifu na umahiri wa hali ya juu, ili kuhakikisha kuwa tunakidhi matarajio ya Watanzania katika sekta hii ya elimu ambayo ndiyo uti wa mgongo wa maendeleo ya taifa letu.

3. **Mheshimiwa Spika,** naomba nitumie fursa hii kumpongeza sana Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa Awamu ya Tano. Aidha nampongeza kwa uongozi wake wenye kuzingatia uwajibikaji na utendaji wenye tija kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuwatumikia kwa moyo wa dhati wananchi wote.

4. **Mheshimiwa Spika,** Napenda pia kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuchaguliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa kuandika historia muhimu sana ya kuwa Makamu wa kwanza mwanamke tangu nchi yetu ilipopata uhuru. Vilevile, nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa, kwa kuteuliwa na Rais na baadaye kuthibitishwa na Bunge lako kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, nawapongeza Mheshimiwa Job Ndugai (Mb) na Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson (Mb) kwa kuchaguliwa kuwa Spika na Naibu Spika wa Bunge hili la 11 pamoja na Wenyeviti wote wa Bunge.

5. **Mheshimiwa Spika,** napenda pia kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kipindi cha Pili na Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi kuwa Makamu wa Pili wa Rais.

6. **Mheshimiwa Spika,** ninapenda kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Peter Serukamba, kwa ushauri mzuri waliotupatia wakati wa maandalizi ya Bajeti hii. Wizara yangu imezingatia na itaendelea kuzingatia ushauri na maelekezo ya Kamati kwa lengo la kuleta ufanisi katika utendaji wa Sekta ya Elimu, Sayansi, na Teknolojia. Aidha, napenda kumshukuru Waziri kivuli wa Wizara hii, Mheshimiwa Susan Lyimo, kwa ushirikiano wake.

7. **Mheshimiwa Spika,** Hotuba yangu imegawanyika katika sehemu kuu Saba: Sehemu ya Kwanza ni Utangulizi; Sehemu ya Pili ni Dira, Dhima na Majukumu ya Wizara; Sehemu ya Tatu ni Vipaumbele vya Wizara kwa mwaka 2016/17; Sehemu ya Nne ni Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2015/16; Sehemu ya Tano ni Mapitio ya Utekelezaji kwa mwaka 2015/16 na Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2016/17; Sehemu ya Sita ni Shukrani; na sehemu ya Saba ni Maombi ya Fedha.

## 2.0 DIRA, DHIMA NA MAJUKUMU YA WIZARA YA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI

### DIRA NA DHIMA YA WIZARA

8. **Mheshimiwa Spika**, Dira ya Wizara ni kuwa na Mtanzania aliyeelimika na mwenye maarifa, stadi, umahiri, uwezo na mitazamo chanya ili kuweza kuchangia katika kuleta maendeleo ya Taifa. Aidha, Dhima ya Wizara ni kuinua ubora wa elimu na mafunzo na kuweka mifumo na taratibu zitakazowezesha kupata idadi kubwa ya Watanzania walioelimika na wanaopenda kujielimisha zaidi ili waweze kuchangia katika kufikia malengo ya maendeleo ya Taifa letu.

### MAJUKUMU YA WIZARA

9. **Mheshimiwa Spika,** Majukumu ya Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi ni kama ifuatavyo:

   (i) kutunga na kutekeleza Sera za Elimu, Utafiti, Huduma za Maktaba, Sayansi, Teknolojia, Ubunifu na Uendelezaji wa Mafunzo ya Ufundi;

   (ii) kuendeleza Elimumsingi kwa Kutoa Ithibati ya Mafunzo ya Ualimu na Maendeleo ya Kitaalamu ya Walimu;

   (iii) kubainisha Vipaji na Kuviendeleza;

(iv) kusimamia Uendelezaji wa Mafunzo katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi;

(v) kusimamia Mfumo wa Tuzo wa Taifa;

(vi) kuainisha Mahitaji ya Nchi katika Ujuzi na Kuuendeleza;

(vii) kuweka Viwango vya Taaluma ya Ualimu;

(viii) kusimamia Ithibati na Uthibiti wa Shule;

(ix) kusimamia Huduma za Machapisho ya Kielimu;

(x) kutegemeza/kuimarisha utumiaji wa Sayansi, Uhandisi, Teknolojia na Hisabati;

(xi) kuendeleza Wataalamu wa ndani katika Sayansi, Teknolojia na Ubunifu;

(xii) kuratibu utafiti katika Sayansi na Teknolojia;

(xiii) uendelezaji wa Rasilimaliwatu na Uongezaji Tija ya Watumishi walio chini ya Wizara; na

(xiv) kuratibu Shughuli za Idara, Mashirika, Wakala, Programu na Miradi iliyo chini ya Wizara.

## 3.0 VIPAUMBELE VYA WIZARA YA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI

10. **Mheshimiwa Spika**, Dira ya Maendeleo ya Taifa (2025) imelenga kuifanya Tanzania kuwa nchi ya kipato cha kati ifikapo mwaka 2025. Katika juhudi za kufikia lengo hili, Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi ina jukumu la kuandaa wataalamu wenye ujuzi na maarifa watakaotoa mchango wenye tija kwa maendeleo ya nchi yetu. Wizara yangu inatambua kuwa utekelezaji wa azma ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kuwa na uchumi wa viwanda inategemea kwa kiasi kikubwa ufanisi katika Sekta ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Ubora wa rasilimali watu ni jambo la msingi sana katika kuhakikisha kuwa tija na ufanisi vinakuwepo katika Sekta zote muhimu ili kuchochea kasi ya ukuaji uchumi na hatimaye kuiwezesha nchi yetu kufikia uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025.

11. **Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia mwelekeo huo, katika mwaka 2016/17, vipaumbele vya Sekta ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi ni kama ifuatavyo:

(i) kuinua ubora wa elimu na mafunzo katika ngazi zote za elimu na mafunzo nchini;

(ii) kuimarisha mifumo na usimamizi wa Ithibati na Uthibiti wa Ubora wa Elimu na mafunzo;

(iii) kuongeza upatikanaji na ushiriki katika fursa za elimu na mafunzo; na

(iv) kuimarisha tafiti na matumizi ya Sayansi, Teknolojia na Ufundi kwa lengo la kuongeza chachu ya maendeleo.

## 4.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA 2015/16

12. **Mheshimiwa Spika,** naomba nianze kutoa tathmini ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2015/16 kuanzia tarehe 1 Julai, 2015 hadi tarehe 30 Aprili, 2016.

### Ukusanyaji wa Maduhuli Kwa Mwaka 2015/16

13. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2015/16, Wizara ilikusudia kukusanya jumla ya **Shilingi 286,074,571,684.47** ambapo Shilingi **9,268,457,100.00** zilitarajiwa kukusanywa na Idara wakati Shilingi **276,806,114,584.47** zilitakiwa kukusanywa na Taasisi zilizo chini ya Wizara. Makusanyo ya maduhuli hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2016 yalikuwa ni jumla ya **Shilingi 199,422,233,349.12** ambayo ni sawa na **asilimia 69.7** ya makadirio. Kati ya fedha hizo, Shilingi **5,723,343,678.36** zilikusanywa na Idara na **Shilingi 193,698,889,670.76** zilikusanywa na Taasisi zilizo chini ya Wizara.

### Matumizi ya Kawaida na Maendeleo kwa Mwaka 2015/16

14. **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2015/16 bajeti ya Wizara ilikuwa ni **Shilingi 1,094,195,824,888.49** (Matumizi ya kawaida

**Shilingi 511,525,227,000.00** na Matumizi ya maendeleo **Shilingi 582,670,597,888.49)**. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2016 fedha ambazo zimekwishatolewa na Hazina zilikuwa **Shilingi 789,460,338,381.61 (**Matumizi ya kawaida **Shilingi 351,284,829,898.00** na Matumizi ya Maendeleo **Shilingi 438,175,508,483.61**) sawa na **asilimia 72.15** ya bajeti ya Wizara. Aidha, fedha zilizotumika hadi kufikia tarehe 30 Aprili 2016 zilikuwa ni **Shilingi 694,148,943,065.89** (Matumizi ya kawaida **Shilingi 313,796,049,657.61** na Matumizi ya maendeleo **Shilingi 380,352,893,408.28)** sawa na **asilimia 87.9** ya fedha zilizotolewa.

## 5.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU KWA MWAKA 2015/16 NA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2016/17

15. **Mheshimiwa Spika,** mwaka 2015/16, Wizara ililenga kusimamia utekelezaji wa mambo makuu yafuatayo:

(i) utungaji na utekelezaji wa Sera za Elimu;

(ii) upatikanaji wa fursa za elimu na mafunzo;

(iii) ithibati ya Shule;

(iv) uthibiti ubora wa elimu;

(v) mafunzo ya Ualimu, hususan wa Sayansi, Hesabu, Ufundi (ikiwemo ufundi sanifu maabara), Lugha na KKK;

(vi) uratibu wa shughuli za Taasisi na Wakala; na

(vii) usimamizi wa utekelezaji wa programu na miradi mbalimbali.

### 5.1 UTUNGAJI NA UTEKELEZAJI WA SERA YA ELIMU

16. **Mheshimiwa Spika,** mojawapo kati ya majukumu ya msingi ya Wizara yangu ni kubuni na kutunga Sera mbalimbali za kusimamia Elimu, Mafunzo ya Ufundi, Sayansi, Teknolojia, Ubunifu, Huduma za Maktaba na Utafiti.

**Utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo (2014)**

**17. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2015/16, yafuatayo yalifanyika:

(i) kutafsiri Sera ya Elimu na Mafunzo (2014) kwa lugha ya Kiingereza na kukamilisha maandalizi ya Mkakati wa Utekelezaji wa Sera ya Elimu;

(ii) kufanya uchambuzi wa mahitaji ya mabadiliko ya sheria ili kutekeleza Sera ya Elimu na Mafunzo (2014);

(iii) kuhuisha mitaala ya elimu ya awali, elimu ya msingi na elimu ya sekondari. Aidha, vitabu vya kiada vya Darasa la Kwanza vinavyoendana na Mtaala uliohuishwa vinasambazwa kwenye Mikoa na Halmashauri zote nchini; na

(iv) ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

**Utekelezaji wa Elimumsingi bila Malipo**

**18. Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza azma ya Serikali ya kutoa Elimumsingi bila Malipo, Wizara yangu ilitoa Waraka wa Elimu Namba 6 wa mwaka 2015 kwa lengo la kutoa mwongozo wa namna ya kutekeleza Elimumsingi bila malipo. Waraka wa Elimu Na. 6 umeweka bayana majukumu ya wadau wote muhimu katika utoaji wa Elimumsingi bila Malipo ambapo imeainishwa kuwa wazazi

wanatakiwa kufanya yafuatayo:

(i) kununua sare za shule na michezo, vifaa vya kujifunzia, chakula kwa wanafunzi wa kutwa na kugharamia matibabu kwa watoto wao.

(ii) kulipia nauli ya kwenda shule na kurudi kwa wanafunzi wa kutwa.

(iii) kulipa nauli za wanafunzi wakati wa likizo; kununua vifaa kwa ajili ya malazi shuleni na vifaa vya kujifunzia.

**19.** **Mheshimiwa Spika**, natoa wito kwa wazazi na walezi kuunga mkono juhudi za Serikali za kuhakikisha kuwa watoto wote wanapata elimu. Ni muhimu wazazi mkawawezesha watoto wenu kupata mahitaji ya shule na muhimu zaidi mjenge utamaduni wa kukagua madaftari ya watoto wenu ili kujiridhisha kama wanafundishwa shuleni.

**20.** **Mheshimiwa Spika**, serikali hutoa fedha ya chakula kwa wanafunzi wa bweni tu. Hivyo, kama kuna shule za sekondari ambazo zimesajiliwa kama shule za kutwa lakini wamejenga Hosteli na miundombinu inayokidhi vigezo vya kuwa shule za bweni, Maafisa Elimu wazitambue na wawasilishe maombi kwenye Wizara yangu ya kuomba kuzibadilisha hadhi. Endapo zitakuwa zimekidhi vigezo muhimu zitabadilishwa na kuwa shule za bweni. Kwa kufanya hivyo, wanafunzi wataweza kutengewa

fedha ya chakula kama ilivyoainishwa kwenye Waraka wa Elimu Na. 6 wa mwaka 2015.

**Mpango wa Utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo (2014) kwa mwaka 2016/17**

**21.** **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/17, Wizara yangu itaendelea na utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo (2014) na Mkakati wake. Wizara itafanya mabadiliko ya Sheria ya Elimu na kupitia Sheria, Kanuni na Taratibu za taasisi zilizo chini ya Wizara, hususan Baraza la Mitihani, Taasisi ya Elimu Tanzania, Taasisi za Ithibati na Uthibiti, Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu na Mamlaka ya Elimu Tanzania kwa lengo la kuimarisha utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo (2014) kwa ufanisi. Aidha, Wizara itakamilisha taratibu za uundwaji wa Bodi ya Kitaalamu ya Walimu.

**22.** **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2016/17, Wizara yangu itaendelea kuimarisha Mpango wa matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji. Vilevile, Wizara itatoa mwongozo wa kuwatambua na kuwaendeleza wanafunzi wenye vipaji, vipawa na mahitaji maalumu na wenye kasi kubwa ya kujifunza masomo ya Sayansi na Hisabati ili kuweza kuwaendeleza katika fani mbalimbali za teknolojia.

### Sera ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu

23. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2016/17, Wizara yangu imedhamiria kuimarisha na kuongeza kasi ya ukuaji wa Sayansi, Teknolojia na Ubunifu kwa kukamilisha mapitio ya Sera zifuatazo:

(i) Sera ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia ya mwaka 1996 na kutunga sera mpya ya Taifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu;

(ii) Sheria Na. 7 ya mwaka 1986 iliyoanzisha Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) na kutunga sheria mpya ya Maendeleo ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu; na

(iii) Sheria Na. 7 ya mwaka 2003 iliyoanzisha Tume ya Nguvu za Atomiki (Tanzania Atomic Energy Commission - TAEC).

## 5.2 UPATIKANAJI WA FURSA ZA ELIMU NA MAFUNZO

### Udahili wa wanafunzi vyuoni

24. **Mheshimiwa Spika**, Serikali ina lengo la kuendelea kuongeza fursa za Elimu na Mafunzo ili kuandaa rasilimali watu itakayochangia maendeleo ya taifa. Kupitia Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, Wizara iliendelea kuratibu udahili wa wanafunzi ambapo kwa mwaka 2015 wanafunzi

189,687 walidahiliwa katika vyuo mbalimbali vya ufundi. Aidha, kwa kupitia Baraza la Elimu ya Ufundi wanafunzi 75,186 walidahiliwa kwenye vyuo mbalimbali kupitia mfumo wa pamoja wa udahili.

25. **Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu kupitia Tume ya Vyuo Vikuu imeendelea kuratibu udahili wa wanafunzi wanaojiunga na Elimu ya Juu kupitia Mfumo wa Udahili wa Pamoja (Central Admission System) wa kudahili wanafunzi wa Digrii ya kwanza. Katika mwaka 2015/16 wanafunzi 65,064 wa Digrii ya kwanza walidahiliwa wakiwemo wanawake 22,225 sawa na asilimia 34.2 na kufanya jumla ya wanafunzi wote wa elimu ya juu kufikia 210,000**.** Wanafunzi hao walidahiliwa katika vyuo vikuu na vyuo vikuu vishiriki 49 na Taasisi zisizo vyuo vikuu 21 (kama ilivyo kwenye kiambatisho Na. 1).

**Elimu Maalum**

26. **Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia kwamba elimu ni haki ya msingi ya kila Mtanzania, Wizara yangu imeendelea kupanua fursa za elimu na mafunzo kwa kuimarisha elimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum. Katika mwaka 2015/16, Wizara yangu iliendesha mafunzo kwa walimu 142 kuhusu ufundishaji wa Sayansi na Hisabati kwa wanafunzi wasioona. Aidha, kupitia Chuo Kikuu Huria cha Tanzania wanafunzi 45 viziwi na wasioona walipewa mafunzo ya kutumia TEHAMA katika kurahisisha

kujifunza ili waweze pia kupata maarifa na taarifa mbalimbali zilizoko kwenye mtandao.

**27.** **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/17 Wizara yangu itafanya yafuatayo:

(i) kununua vifaa mbalimbali vya wanafunzi wenye mahitaji maalum. Vifaa hivyo ni pamoja na mashine za nukta nundu, fimbo nyeupe, viti vya magurudumu, visaidizi vya kusikia, na vifaa vya vituo maalum vya msaada wa kitabibu;

(ii) kukarabati na kufanya matengenezo ya vifaa vya wanafunzi walemavu; na

(iii) kuwezesha upatikanaji wa vifaa vya maabara na vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum wa shule za msingi na Sekondari.

## 5.3 KUINUA UBORA WA ELIMU NA MAFUNZO

**28.** **Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu inatambua kwamba elimu bora ina nafasi ya pekee katika kufanikisha ujenzi wa msingi wa uchumi wa kisasa wa taifa linalojitegemea. Ili kukidhi azma hii, Wizara yangu imeimarisha na kuboresha mfumo wa ithibati na uthibiti wa shule na vyuo, mafunzo ya ualimu, mazingira ya kufundishia na kujifunzia pamoja na huduma za maktaba.

### Ithibati ya Shule za Msingi na Sekondari

29. **Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu imeendelea kusimamia ithibati ya shule kwa lengo la kuzipatia shule idhini ya kufundisha masomo husika, kuthibitisha Wamiliki na Mameneja wa Shule na kutoa vibali vya ujenzi wa shule zisizo za Serikali. Hadi kufikia Aprili, 2016 shughuli zifuatazo zilifanyika:

(i) shule 174 zikiwemo shule za awali 4, msingi 115 na sekondari 55 zilisajiliwa;

(ii) kutoa vibali kwa Wamiliki 151 na Mameneja 154 wa shule na vibali vya ujenzi wa shule 201 zisizo za Serikali;

(iii) kufuta vibali vya ujenzi kwa shule 37 kwa kuwa vilikuwa vimeombwa zaidi ya miaka kumi iliyopita, na hapakuwa na jitihada za kuendelea na ujenzi na kuanza taratibu za kusajili shule hizo; na

(iv) Wamiliki na Mameneja wa shule 13 walifutiwa uthibitisho kutokana na shule zao kubadili umiliki.

30. **Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka 2016/17, Wizara yangu itafanya yafuatayo katika ithibati ya shule;

(i) kuhuisha na kuandaa Mwongozo wa Usajili wa Shule za Serikali na zisizo za Serikali kulingana na mahitaji ya sasa;

(ii) kusajili shule za Awali, Msingi na Sekondari kwa kutilia mkazo uanzishwaji wa shule zenye mwelekeo wa Sayansi, Kilimo, Teknolojia na Ufundi; na

(iii) kusajili vituo vinavyotoa Elimu Nje ya Mfumo Rasmi na Elimu Huria.

**Uthibiti wa Ubora wa Shule za Msingi na Sekondari**

**31.** **Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu inatambua kwamba, uthibiti ubora wa shule ni jambo muhimu sana katika kuimarisha ubora wa elimu na mafunzo yanayotolewa katika shule za msingi na sekondari. Hadi kufikia Aprili, 2016, shule 7,882 kati ya 17,242 ambayo ni sawa na asilimia 46 ya shule zilizolengwa zilifanyiwa ukaguzi. Aidha, walimu 292 waliteuliwa kuwa Wathibiti Ubora wa Shule na kupangwa katika ofisi za Kanda na Wilaya kwa lengo la kuimarisha ukaguzi wa shule.

**32.** **Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu inafuatilia kwa karibu na kuhakikisha kwamba watoto wote wanafundishwa vema na wanaweza kumudu stadi za kusoma, kuandika na kuhesabu (KKK) kuanzia hatua za mwanzo. Katika kutimiza azma hii Wathibiti Ubora wa Shule wapatao 1,435 wamepatiwa mafunzo ya stadi za kufundisha KKK ili waweze kufuatilia utekelezaji wake katika shule za msingi na kutoa msaada kwa walimu wanapofundisha.

Vilevile, Wizara ilifungua ofisi za Uthibiti Ubora wa Shule na kupeleka Wathibiti Ubora wa Shule katika Halmashauri za Wanging'ombe, Makambako, Kaliua, Nyasa, Geita (Mji), Njombe (Mji), Nyangh'wale, Ikungi, Kalambo, Mbogwe, Buligwe, Gairo, Chemba, Majinga, Momba, Bumbuli, Handeni (M), na Mkarama. Ofisi hizi zimesaidia walimu na wadau wa elimu kupata huduma za Wathibiti Ubora wa Shule kwa karibu zaidi.

33. **Mheshimiwa Spika,** katika uthibiti ubora wa shule kwa mwaka 2016/17, Wizara imepanga kufanya yafuatayo:

(i) kufuatilia ubora wa utoaji elimu katika shule 10,818 na kutoa ushauri kwa lengo la kuboresha ufundishaji;

(ii) kutoa ushauri wa kitaalamu na kitaaluma kwa wadau wa elimu;

(iii) kukamilisha ujenzi wa ofisi za uthibiti ubora katika Wilaya za Hai, Masasi, Mtwara Mjini, Namtumbo, Urambo na Sumbawanga Mjini;

(iv) kufuatilia ufundishaji katika elimu ya awali na stadi za KKK kwa wanafunzi wa Darasa la I na II;

(v) kuandaa kiunzi cha Uthibiti Ubora wa Shule (Basic Education Quality Assurance Framework) na kutekeleza mapendekezo ya

uimarishaji wa mfumo wa ukaguzi;

(vi) kuhuisha mwongozo wa Wathibiti Ubora, kuchapa na kusambaza kwa Wathibiti Ubora wote; na

(vii) kununua na kugawa pikipiki kwa Waratibu Elimu Kata wa Mikoa 18 na kuchangia mafuta kwa ajili ya magari na pikipiki zilizonunuliwa chini ya Mpango wa LANES.

**Ithibati na Uthibiti wa Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi**

**34.** **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka 2015/16, Wizara yangu iliendelea kusimamia ubora wa Elimu ya Ufundi nchini kwa kupitia Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi. Baraza lilivifanyia tathmini na kuvisajili vyuo 70, kutoa ithibati kwa Vyuo 23 vya Ufundi; na kuhakiki jumla ya Wakufunzi 807 ili kubaini uhalali wao wa kufundisha katika ngazi husika. Aidha, Baraza limetambua Idara 35 na kuzipatia ithibati ya kuendesha programu za mafunzo.

**35.** **Mheshimiwa Spika,** ili kuimarisha elimu ya ufundi nchini, Baraza liliendesha mafunzo ya kuhakiki ubora wa mafunzo vyuoni kwa wafanyakazi 30 wa Baraza na kwa wakufunzi 22 wa vyuo pamoja na kukagua jumla ya vyuo 35 ili kutathmini ubora wa utoaji wa mafunzo. Aidha, Baraza liliidhinisha mitaala 93 inayozingatia umahiri ikiwemo 42 ya

ngazi ya Cheti, 34 ya Diploma, 16 ya Digrii na 1 Digrii ya uzamili. Baraza pia limetoa mafunzo ya jinsi ya kutumia mitaala inayozingatia umahiri kwa wakufunzi 417 wa vyuo.

**36.** **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2016/17, Wizara yangu kupitia Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi itaendelea kukagua na kusajili vyuo vya ufundi kulingana na maombi na mahitaji ya nchi. Baraza pia litaendelea kusajili wakufunzi ili kuhakiki sifa zao pamoja na kukagua na kutoa ithibati kwa vyuo vya ufundi na kutambua idara zenye uwezo wa kuendesha programu mbalimbali za ufundi.

**37.** **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2016/17, Wizara yangu pia kupitia Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi litafanya shughuli zifuatazo:

(i) tathmini ya ubora wa mafunzo katika vyuo 60 na kuboresha miongozo na taratibu za usajili na utoaji ithibati kwa vyuo vya ufundi.

(ii) litadahili wanafunzi 90,000 katika ngazi ya Cheti, Diploma na Digrii kupitia mfumo wa pamoja wa udahili.

(iii) litajengea uwezo vyuo 60 katika kujihakiki na kusimamia ubora wa mafunzo vyuoni, kupima na kuhakiki ubora wa mitaala ya vyuo vya ufundi katika ngazi zote,

(iv) litatengeneza mfumo wa kielektroniki wa kupokea na kuhakiki mitaala, kufanya tafiti zenye lengo la kuboresha utoaji wa mafunzo ya elimu ya ufundi,

(v) kuratibu mafunzo ya kutumia mitaala inayozingatia umahiri kwa walimu 400,

(vi) kuandaa moduli za mafunzo kwa walimu kuhusu kuandaa, kupitia, kufundisha na kupima mitaala ya elimu ya ufundi.

**Uthibiti Ubora wa Vyuo vya Elimu ya Juu**

**38.** **Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu imeendelea kusimamia ubora wa elimu ya juu kupitia Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania. Katika mwaka 2015/16, Tume ya Vyuo Vikuu ilikagua na kutathmini vyuo vikuu 15 nchini kwa lengo la kusimamia ubora. Katika ukaguzi huo, ilibainika kuwa Chuo Kikuu cha Mt. Yosefu Kampasi ya Songea (Koleji za Kilimo, Teknolojia na TEHAMA) na Kampasi ya Arusha hazikukidhi viwango vya ubora stahiki. Changamoto zilizobainika ni pamoja na vyuo kutokuwa na wahadhiri wenye sifa stahiki na mitaala kutoandaliwa ipasavyo. Mazingira ya kufundishia na kujifunzia kutokidhi vigezo hususan ukosefu wa mafunzo kwa vitendo kutokana na kutokuwepo kwa maabara.

**Kufutwa kwa Ithibati kwa Chuo cha Mt Yosef**

39. **Mheshimiwa Spika**, Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania kwa kutumia mamlaka yake kisheria ilifuta usajili wa Koleji za Songea na Kampasi ya Arusha. Kutokana na hatua hiyo, jumla ya wanafunzi 3,585 waliokuwa kwenye vyuo hivyo walihamishiwa kwenye Vyuo vingine. Hata hivyo, imekuwepo changamoto katika kupokelewa kwa wanafunzi hao kwani vyuo vilivyowapokea vimeona hawakuwa wamesoma kwa kiwango cha kutosha ukilinganisha na mwaka wa masomo waliokuwepo. Ili kuhakikisha wanapata maarifa stahiki kwa miaka waliyopo, baadhi ya vyuo vimewarudisha mwaka wakati vingine vimelazimika kuwapa mafunzo ya ziada kukabiliana na mapungufu kitaaluma waliyoyabaini.

40. **Mheshimiwa Spika,** Hali hiyo inathibitisha kuwa elimu iliyokuwa ikitolewa katika Chuo cha Mt Yosef haikuwa inakidhi viwango hali iliyosababisha kuwepo kwa migogoro ya wanafunzi ya mara kwa mara katika chuo hicho. Napenda kuchukua nafasi hii kuviagiza vyuo vyote vya elimu kuhakikisha vinaendeshwa kwa kufuata Sheria. Kanuni na Taratibu. Wizara yangu haitasita kuchukua hatua kali dhidi ya chuo kitakachokwenda kinyume na taratibu.

**Wanafunzi wa Kidato cha 4 waliokuwa wanachukua** Digrii **Katika chuo cha Mt. Yosef**

41. **Mheshimiwa Spika**, naomba sasa nizungumzie suala la wanafunzi 424 wa Mt Yosef walioondolewa chuoni. Suala hili liliwasilishwa katika Bunge lako tukufu siku ya tarehe 17/05/2015 na Mh Cosato David Chumi (Mbunge wa Mafinga). Kwa mujibu wa Kanuni 28(11) aliwasilisha maelezo binafsi akitaka Serikali kutoa ufafanuzi kuhusu hatua hiyo. Nitatoa ufafanuzi wa kina ili sababu za uamuzi huo ziweze kueleweka ipasavyo.

42. **Mheshimiwa Spika**, katika zoezi la kuwahamisha wanafunzi wa Mt. Yosef kampasi ya Arusha, ilibainika kuwa walikuwepo wanafunzi ambao walidahiliwa kujiunga na Digrii ya Ualimu kwa masomo ya Sayansi wakati hawakuwa na sifa stahiki. Wanafunzi hao walikuwa wamemaliza Kidato cha Nne wakiwa na ufaulu hafifu ambapo mwanafunzi aliyepata ‘D’ nne sawa na Divishen IV ya pointi 31 alipewa fursa ya kudahiliwa kwenye Digrii ya Ualimu wa Sayansi.

43. **Mheshimiwa Spika**, jambo la kusikitisha zaidi ni kuwa katika kudahili wanafunzi hao kwenye Digrii ya Sayansi, masomo ya msingi aliyoyasoma mwanafunzi hayakuzingatiwa. Kwa mfano, wapo waliochukua mkondo wa Biashara yaani masomo ya Book-keeping na Commerce lakini walidahiliwa

kusoma Sayansi. Aidha, wapo ambao hawakuchukua kabisa mkondo wa Sayansi yaani masomo ya Sayansi lakini walidahiliwa. Vilevile, wapo wanafunzi waliofeli masomo ya Sayansi Kidato cha Nne lakini wakadahiliwa kuchukua Digrii ya Sayansi ya Ualimu kama inavyooneshwa katika mifano ifuatayo:

| S/N | INDEX | UFAULU KWA MASOMO |
|---|---|---|
| 1 | S2123/0043/2011 | CIV-D,HIS-F,GEO-D,KIS-F,ENG-D,PHY-D,CHE-F,BIO-D,MAT-F |
| 2 | S0194/0027/2012 | CIV-C,HIS-D,GEO-D,BIB-D,KIS-D,ENG-D,BIO-D,MAT-F,COM-D,BOO-F |
| 3 | S0348/0068/2005 | CIV-D,HIS-F,GEO-D,KIS-F,ENG-D,PHY-F,CHE-D,BIO-D,AGR-F,MAT-F |
| 4 | S0353/0091/2009 | CIV-D,HIS-D,GEO-F,KIS-D,ENG-F,PHY-F,CHE-D,BIO-D,AGR-C,MAT-F |
| 5 | S2295/0019/2012 | CIV-D,HIS-C,GEO-D,KIS-D,ENG-D,BIO-C,COM-D,MAT-F |

**44.** **Mheshimiwa Spika**, kutokana na wanafunzi kuwa na sifa za aina hiyo ambazo hazitoshelezi hata kujiunga na mafunzo ya Cheti cha Ualimu, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Vyuo Vikuu, imefuta udahili wao wa Digrii ya Ualimu wa Sayansi. Serikali imesikitishwa sana na na kitendo hicho cha kudahili wanafunzi hao kujiunga na Digrii ya Ualimu wa Sayansi wakati hawana sifa stahiki. Katika mwaka 2013/14 walipodahiliwa kwa ufaulu wa Kidato cha 4 kwa kiwango cha angalau ‘D’ nne, sifa za kujiunga na Cheti cha Ualimu zilikuwa ziko juu zaidi. Aidha, wanafunzi hao walipewa mikopo licha ya kutokuwa na sifa stahiki.

**45.** **Mheshimiwa Spika**, kutokana na hali hiyo, Serikali imeunda Kamati ya kuchunguza mchakato mzima

wa uanzishwaji wa programu hiyo na sababu za wanafunzi wasio na sifa kudahiliwa. Hatua kali zitachukuliwa dhidi ya wote watakaobainika kuhusika na suala hilo.

**Mafunzo ya Ualimu**

**46.** **Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu inatambua umuhimu wa kuwa na walimu wenye sifa, maarifa na weledi katika kuinua viwango na ubora wa elimu. Katika mwaka 2015/16 Wizara yangu iliendelea na juhudi za kuongeza walimu, hususani walimu wa Sayansi na Hisabati ili kukabiliana na upungufu wa walimu wapatao 22,000 uliopo sasa. Walimu tarajali 5,690 walidahiliwa kwa ngazi ya Diploma ya Ualimu wa masomo ya Hisabati na Sayansi katika Chuo Kikuu cha Dodoma na vyuo vya ualimu vya Kleruu, Monduli na Korogwe. Aidha, Wizara imeendelea kutilia mkazo sifa za kudahili wanafunzi katika programu za Ualimu, ambapo ufaulu wa chini ni Daraja la Tatu katika mtihani wa kuhitimu Kidato cha Nne na Kidato cha Sita.

**47.** **Mheshimiwa Spika,** ili kuimarisha uwezo wa kitaaluma wa wakufunzi wa Sayansi na Hisabati katika vyuo vya ualimu, Wizara yangu kupitia ufadhili wa China Trust Fund na UNESCO – Tanzania imetoa mafunzo ya TEHAMA kwa wakufunzi 20 na kuweka miundombinu ya TEHAMA kwa vyuo vya Monduli na Tabora. Miundombinu hii imeimarisha ufundishaji

na ujifunzaji wa masomo ya Sayansi na Hisabati.

48. **Mheshimiwa Spika** kwa kutambua kwamba wanafunzi wanaojiunga na elimu ya sekondari wanahitaji mafunzo kabilishi ya lugha ya kiingereza, Wizara yangu imetoa mafunzo kwa walimu 2,485 wa shule za sekondari kwa lengo la kuwawezesha walimu hao kumudu kuwasaidia wanafunzi wa Kidato cha Kwanza. Aidha, vitabu 26,000 vya wawezeshaji na walimu vimeandaliwa na kusambazwa kwenye wilaya 37 na mikoa 5 ya majaribio.

49. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2016/17 Wizara yangu itaendelea kutoa mafunzo tarajali (Pre-service) ya walimu wa elimu ya awali pamoja na wale wa masomo ya Ufundi kwa shule za sekondari za ufundi na mafunzo ya Ufundi Sanifu wa Maabara kwa ajili ya maabara za shule za Sekondari. Aidha, Wizara yangu itaendelea kuendesha mafunzo kazini kwa Walimu wa Elimu Maalumu, Elimu ya Ufundi na kwa masomo yote ya Elimumsingi.

**Uboreshaji wa Mazingira ya Kufundishia na Kujifunzia**

**Elimumsingi na Sekondari**

50. **Mheshimiwa Spika,** Mazingira ya kufundishia na kujifunzia yana mchango mkubwa katika kuinua ubora wa elimu katika ngazi zote. Katika mwaka

2015/16, Wizara imeandaa mpango wa ukarabati wa shule kongwe za sekondari nchini ambapo katika Awamu ya Kwanza shule 33 zitakarabatiwa. Shule hizi ni Ihungo, Ilboru, Kilakala, Mwenge, Msalato, Mzumbe, Nganza, Pugu, Same, Tabora Boys na Tabora Girls. Shule nyingine ni Azania, Jangwani, Kantalamba, Mpwapwa, Tosamaganga, Malangali, Milambo, Nangwa, Kibiti, Minaki, Ifakara, Songea Boys, Ndanda, Kigoma, Kibaha na Shule za Ufundi za Bwiru Boys, Ifunda, Iyunga, Moshi, Mtwara, Musoma na Tanga.

**51.** **Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu kwa kushirikiana na wabia wa maendeleo na OR-TAMISEMI imewezesha shule 250 za msingi na sekondari katika wilaya 25 kuunganishwa kwenye mtandao wa "internet" na kupatiwa kompyuta mpakato, Projector na kompyuta endeshi (Server) kwa ajili ya matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji.

**52.** **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2016/17, Wizara yangu kupitia Mamlaka ya Elimu itaendelea na uimarishaji wa miundombinu ya Shule na Vyuo vya Ualimu, ikiwemo ukarabati wa shule za sekondari 7 kongwe pamoja na ujenzi wa nyumba 30 za walimu zenye uwezo wa kuchukua walimu 180, katika maeneo yasiyofikiwa kwa urahisi. Wizara pia itajenga vyumba 25 vya madarasa na matundu 200 ya vyoo katika shule zenye uhitaji mkubwa.

**Elimu ya Juu**

53. **Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu inatambua umuhimu wa mchango wa elimu ya juu katika juhudi za kufikisha nchi yetu katika uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025. Kwa kuzingatia hilo, Wizara yangu imekuwa ikiongeza majengo na kukarabati miundombinu ya Vyuo Vikuu na Taasisi za Elimu ili kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa lengo la kuinua ubora na kuongeza fursa kwa wanafunzi wengi zaidi kujiunga na Elimu ya Juu. Katika mwaka 2015/16 baadhi ya shughuli zilizofanyika katika taasisi za elimu ya juu ni pamoja na:

(i) Kukamilisha ujenzi wa maabara kwa ajili ya Kitivo cha Sayansi- Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo unaogharimiwa na Mradi wa *Enhancing Pro-poor Innovation in Natural Resources and Agricultural Value-chain* (EPINAV). Mradi huu umekamilika kwa asilimia 75. Aidha, Chuo kimekarabati maktaba na maabara na kupeleka maji Kampasi ya Solomon Mahlangu; na

(ii) kukarabati vituo vya Mikoa ya Temeke, Mbeya, Bungo na Kinondoni vinavyosimamiwa na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

**54. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2016/17, Wizara yangu itaendelea kuboresha mazingira ya kufundisha na kujifunzia kwa kufanya yafuatayo:

(i) kukiwezesha Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kukarabati miundombinu katika mikoa ya Ruvuma, Rukwa, Kilimanjaro, Singida, Mara na Pwani;

(ii) kukarabati hosteli za wanafunzi, kumbi za mihadhara, Kituo cha Polisi, nyumba za wahadhiri pamoja na miundombinu ya majitaka katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam;

(iii) kukarabati hosteli za wanafunzi Kampasi kuu na ujenzi wa majengo ya madarasa na ofisi za kampasi ya Mbeya ya Chuo Kikuu cha Mzumbe;

(iv) kujenga maabara katika Chuo Kikuu cha Ardhi ambayo itakuwa na matumizi mbalimbali (Mult-purpose Laboratory) pamoja na kukarabati hosteli za wanafunzi;

(v) kukarabati kumbi za mihadhara, maabara na hosteli za wanafunzi katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo;

(vi) kukarabati majengo na miundombinu mingine katika Kampasi Kuu ya Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi na Kampasi ya Kizumbi;

(vii) kukamilisha ujenzi wa jengo la Utawala na kuanza ujenzi wa Maabara za Sayansi ili kuongeza fursa kwa wanafunzi zaidi kudahiliwa

katika mafunzo ya Sayansi katika Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam;

(viii) kujenga madarasa na Hosteli kwa Chuo cha "Earth Sciences" pamoja na Chuo cha "Natural and Mathematical Sciences" katika Chuo Kikuu cha Dodoma;

(ix) kukamilisha jengo la Mihadhara la Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa na kukarabati miundombinu ya Chuo hicho;

(x) kujenga na kuweka samani katika jengo la Maktaba ya Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya ili kuendana na ongezeko la udahili;

(xi) kukamilisha ujezi wa jengo la ghorofa kumi katika Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam na kuweka umeme na samani katika Kampasi Kuu na kukarabati miundombinu ya majitaka kwa Kampasi ya Mwanza ambayo itaanza kutoa mafunzo katika ngazi ya cheti katika fani ya utunzaji na usindikaji wa ngozi kuanzia hatua ya mnyama akiwa hai, akichinjwa hadi kufikia hatua ya uchunaji na usindikaji wa ngozi; na

(xii) kuendeleza ujenzi wa Hosteli katika Kampasi ya Kivukoni ya Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere na kununua samani kwa ajili ya Kampasi ya Bububu, Zanzibar.

**55.** **Mheshimiwa Spika,** Wizara inaendelea na mpango wa uanzishwaji wa Chuo Kikuu cha Kilimo na Teknolojia cha Mwalimu Julius K. Nyerere. Utaratibu wa ujenzi wa Kampasi kuu ya Butiama utaanza mwaka wa 2016/17. Kuhusu kutumia majengo ya Shule ya Sekondari Oswald Mang'ombe, Wizara imefanya mazungumzo na wamiliki kukamilisha uhamishaji wa miliki ya majengo kisheria. Aidha, tunawashukuru wamiliki pamoja na Mheshimiwa Nimrod Mkono kwa mchango wao katika kukuza elimu nchini.

**Kampasi Mpya ya Mloganzila**

**56.** **Mheshimiwa Spika,** napenda kutoa taarifa kuwa ujenzi wa hospitali ya kufundishia ya Kampasi mpya ya Mloganzila ya Chuo cha Afya na Sayansi Shirikishi cha Muhimbili (MUHAS) iliyojengwa kwa ushirikiano wa Serikali yetu na Serikali ya Korea Kusini inatarajiwa kukamilika mwezi Juni 2016. Hospitali hii itakuwa na uwezo wa kubeba wagonjwa 571 wa kulazwa kwa wakati mmoja.

**57.** **Mheshimiwa Spika,** pamoja na juhudi za Serikali kukamilisha Awamu ya Kwanza ya ujenzi wa hospitali hii, bado kuna changamoto ya majengo mengine ya chuo kama madarasa, maabara, maktaba, majengo ya utawala, mabweni ya wanafunzi, nyumba za wafanyakazi n.k. Majengo haya ni muhimu ili Kampasi hii ya Chuo ikamilike na

hivyo Chuo kiweze kuongeza udahili wa wanafunzi kutoka 3,000 wa sasa na kufikia wanafunzi 15,000 kitakapokamilisha Awamu ya Pili. Katika mwaka 2016/17 Wizara inalenga kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza awamu ya pili ya ujenzi ambapo tayari andiko la kutafuta fedha kutoka kwa wafadhili na wawekezaji limeandaliwa.

**Ujenzi wa Kituo Mahiri cha Magonjwa ya Moyo – Mloganzila**

**58.** **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2016/17 Wizara yangu itaanza ujenzi wa Kituo Mahiri cha Magonjwa ya Moyo na Mishipa ya Damu cha Afrika Mashariki katika eneo la Mloganzila.

**Huduma za Maktaba**

**59.** **Mheshimiwa Spika,** huduma bora za Maktaba zinachangia katika utoaji wa Elimu bora katika nchi yoyote ile. Wizara yangu kupitia Bodi ya Huduma za Maktaba ina jukumu la kuanzisha, kusimamia, kuongoza, kuimarisha, kutunza na kuendeleza Maktaba za Umma. Uendelezaji wa huduma za Maktaba, unaanzia ngazi ya Kijiji, Wilaya hadi Mkoa pamoja na kutoa mafunzo na kuendesha mitihani ya Taaluma ya Ukutubi. Katika mwaka 2015/16 Wizara kupitia Bodi ya Huduma za Maktaba imefanya yafuatayo:

(i) imeendelea kuimarisha huduma za Maktaba kwa kusambaza vitabu vya rejea 68,000 kwa masomo yote katika maktaba za mikoa.

(ii) imetoa ushauri wa kitaalamu kuhusu uanzishaji na uendeshaji wa Maktaba katika shule 28 (17 za msingi na 11 za sekondari), vyuo 5 na Halmashauri za Wilaya 4 ambazo ni Mkinga, Longido, Kongwa na Ushirombo.

**60.** **Mheshimiwa Spika**, ili kukabiliana na upungufu wa wataalam wa Maktaba katika asasi na taasisi za elimu nchini, Wizara kupitia Chuo cha Ukutubi na Uhifadhi Nyaraka (SLADS) Bagamoyo, imeratibu utoaji wa mafunzo kwa wanafunzi 1,363; wakiwemo Cheti 390; Diploma 773 na kozi ya miezi mitatu "*Elementary Library Course*" 200. Wanafunzi hawa watakapohitimu wataongeza idadi ya wataaalam wa Maktaba katika maeneo yaliyo na uhitaji mkubwa wa wakutubi, ikiwa ni pamoja na Shule, Vyuo vya Ualimu na Maktaba za Umma. Aidha, ukarabati mdogo umefanyika katika Maktaba za mkoa wa Mtwara na Tanga.

**61.** **Mheshimiwa Spika**, naomba nitumie fursa hii kutoa wito kwa Halmashauri zote nchini pamoja na wadau kuona umuhimu wa kuanzisha maktaba na kuhamasisha wananchi kujenga utamaduni wa kusoma vitabu, vijarida na machapisho mbalimbali. Wizara yangu iko tayari kutoa ushauri wa kitaalamu

kuhusu uanzishwaji na uendeshaji wa maktaba.

62. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2016/17, Wizara kupitia Bodi ya Huduma za Maktaba itafanya yafuatayo:

(i) itaimarisha na kuinua ubora wa huduma za maktaba katika mikoa 21 kwa kuongeza machapisho/vitabu 40,000 ya watu wazima na watoto ili kuongeza ari ya usomaji katika jamii;

(ii) itatoa ushauri wa kitaalamu juu ya uanzishaji na uendeshaji wa Maktaba za Shule, Vyuo, Taasisi na Halmashauri za Miji, Manispaa na Wilaya nchini;

(iii) itatoa mafunzo ya Ukutubi na Uhifadhi Nyaraka kwa walengwa 700 wa Cheti, 700 wa Diploma na 500 wa mafunzo ya muda mfupi kwa ajili ya wafanyakazi wa Maktaba;

(iv) itaendeleza miundombinu ya Chuo cha Ukutubi na Uhifadhi Nyaraka (SLADS), Bagamoyo kwa kujenga maktaba ya chuo pamoja na kukarabati majengo ya maktaba za Tabora, Tanga na Rukwa; na

(v) itaanza matayarisho ya ujenzi wa majengo ya maktaba za mikoa ya Singida na Shinyanga ili kutoa fursa kwa wananchi wa mikoa hiyo kupata machapisho na huduma nyingine za maktaba za umma.

## 5.4 TAFITI NA HUDUMA KWA JAMII

### Utekelezaji wa Tafiti na Huduma 2015/16

63. **Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu ina jukumu la kufanya tafiti na kutoa huduma kwa jamii kupitia Vyuo Vikuu na Taasisi za Elimu ya Juu. Katika mwaka wa fedha 2015/2016, Wizara yangu kupitia Vyuo Vikuu imefanya tafiti mbalimbali zenye matokeo makubwa kwa jamii kama ifuatavyo:

### Chuo Kikuu cha Sokoine

(i) udhibiti wa magonjwa ya mifugo yaletwayo na kupe, mbung'o na minyoo kwa wafugaji wa asili, ambapo wafugaji hao sasa wamefanikiwa kuongeza kipato kutokana na kupungua kwa magonjwa ya mifugo yao;

(ii) kutumia Panya Buku kutatua matatizo ya jamii ikiwa ni pamoja na kutambua wagonjwa ya kifua kikuu kwa kasi kubwa na kwa usahihi zaidi ya darubini. Aidha, utafiti umegundua kuwa wanyama hao wanafundishika na wanao uwezo wa kutumika kutegua mabomu katika jamii zilizokumbwa na vita. Panya hao wameweza kutegua mabomu katika nchi za Cambodia, Msumbiji, Jamhuri ya Lao, Vietnam na Thailand, ambapo nchi hizo sasa zimetangaza kwamba hazina tena tishio la

mabomu baada ya kuwatumia panya hao; na

(iii) uzalishaji wa mbegu bora za maharage zenye kustahimili magonjwa na ukame, kuzaa vizuri na kuiva kwa muda mfupi. Matokeo ya utafiti huu yamesambazwa kwa wakulima ambapo wanatumia mbegu bora za maharage (SUA 90, ROJO, Mshindi na Pesa) na wameweza kuongeza uzalishaji na kipato chao.

**Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili**

(i) utafiti wa majaribio ya chanjo ya VVU awamu ya II, uliohusisha nchi za Tanzania na Msumbiji (Tanzania Mozambique Vaccine – TaMoVac II). Chanjo hii ilijaribiwa na kuthibitishwa kuwa salama na ina uwezo wa kufanya mwili utengeneze viashiria vya kinga. Pia majaribio hayo yamewezesha wanasayansi kubaini dozi sahihi ya chanjo na namna ya kuitoa ili iweze kufanya kazi katika kiwango kinachotakiwa;

(ii) matibabu ya ugonjwa wa Malaria na kuboresha mfumo wa matibabu ya ugonjwa kwa lengo la kupunguza athari zitokanazo na Malaria hasa kwa akina mama wajawazito na watoto; na

(iii) ugonjwa wa Selimundu ambapo utafiti huo umebaini mbinu bora zaidi za kuhudumia wenye tatizo hilo.

**Chuo Kikuu cha Dar es Salaam**

Tafiti zifuatazo zilifanyika:

(i) ufuatiliaji wa mienendo ya Tembo kwa kutumia teknolojia ya GPS (Global Positioning System) inayoonesha mahali tembo alipo kwa wakati wote. Matokeo ya utafiti huu yanasaidia kukabiliana na tatizo la ujangili wa tembo. Utafiti huu umewezesha ulinzi wa tembo kufanyika kwa ufanisi mkubwa zaidi;

(ii) utafiti kuhusu kilimo cha uyoga pori kwa matumizi ya chakula na biashara, ambao umewezesha wakulima wapatao 4,000 kulima aina tano za uyoga na hivyo kuongeza uzalishaji wa zao hili na kujiongezea kipato; na

(iii) ufugaji wa samaki wa maji baridi aina ya Tilapia katika maji chumvi ambao umewasaidia wakulima wa Rufiji kuweza kufuga aina hii ya samaki katika maeneo yao na hivyo kuongeza kipato cha kaya.

**64.** **Mheshimiwa Spika**, Napenda kuchukua fursa hii kuwajulisha wananchi na wadau mbalimbali wanaweza kusoma na kuona matokeo ya tafiti hizo kwenye tovuti za vyuo husika.

## Malengo ya Tafiti na Huduma 2016/17

65. **Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu kupitia vyuo vikuu itaendelea kufanya tafiti na kutoa ushauri kwa jamii kwa kutumia fedha za Serikali na wadau wa maendeleo. Katika mwaka 2016/17 baadhi ya tafiti zitakazofanyika zitakuwa kama ifuatavyo:

(i) Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kitaendelea kusimamia miradi 12 ya utafiti inayofadhiliwa na Sida kuhusu rasilimali maji (water resources); sayansi za bahari na rasilimali zake; usalama wa chakula (Food Security); mabadiliko ya tabianchi; utalii; biashara ya rasilimali za kilimo; kujenga uwezo katika Hisabati, na Sayansi za Molekali Biolojia (Molecular Biosciences) na “Nishati Joto”;

(ii) Chuo Kikuu cha Ardhi, kitafanya tafiti na kutoa ushauri wa kitaalam kuhusu matumizi bora ya ardhi, ujenzi, usanifu majengo na usimamizi wa mazingira;

(iii) Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi, kitafanya tafitina kutoa ushauri wa kitaalam na kuchapa makala kwa lengo la kusambaza elimu inayokidhi mahitaji ya sasa ya jamii ili kupunguza umaskini;

(iv) Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi cha Muhimbili, itaendelea na tafiti za: afya ya akina mama na watoto, majaribio ya chanjo dhidi ya

maambukizi ya VVU, uchunguzi wa kifua kikuu (TB); malaria; magonjwa makuu ya tropiki yasiyopewa kipaumbele (Neglected Tropical Diseases) na magonjwa yasiyoambukiza (magonjwa ya moyo, kisukari, selimundi n.k); na

(v) Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) na Taasisi ya Afrika ya Nelson Mandela ya Sayansi na Teknolojia (NM-AIST) vitafanya tafiti nne ambazo zinaviandaa kuwa vituo mahiri vya utafiti na taaluma katika Ukanda wa Afrika Mashariki na Kusini. Tafiti hizo ni SUA (*Innovative Rodent Management and Biosensor Technology Development*; na *Infectious Disease Surveillance*) na NM-AIST (Miundombinu ya Maji na Nishati Endelevu; na ya pili ni kuhusu Maendeleo na Elimu Endelevu ya Kilimo).

## 5.5 SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UBUNIFU

**66. Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu inatambua umuhimu wa Sayansi, Teknolojia na Ubunifu pamoja na matumizi yake katika kuleta maendeleo ya nchi. Wizara imefanya yafuatayo katika mwaka 2015/16:

(i) imekamilisha uandaaji wa Mpango wa Maendeleo ya Sayansi na Teknolojia na mkakati wa utekelezaji ambao uliandaliwa kupitia mpango wa Matokeo Makubwa Sasa.

(ii) imesimamia majadiliano ya Mkataba wa Ushirikiano kati ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya Zambia katika masuala ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu na kufanya Mikutano ya kuhamasisha umuhimu wa kuwa na dawati la sayansi, teknolojia na ubunifu kwa wadau.

(iii) iliendesha Kambikazi ya Maabara ambapo matokeo yake yamekuwa msingi wa kuandaa programu za utekelezaji wa mpango wa maendeleo ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu.

(iv) katika kuongeza idadi ya wanafunzi wa kike wanaojiunga na masomo ya Sayansi, Wizara yangu pia iliendesha mafunzo maalumu ya kuongeza uwezo wa kitaaluma wa wanafunzi wa kike 305 ambao hatimaye walijiunga na kozi katika Vyuo vya Elimu ya Juu na Ufundi vitano (5) vya Tanzania Bara na Zanzibar.

**67.** **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2016/17, Wizara yangu imepanga kuanzisha maabara na kupanua vituo vya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu pamoja na kufadhili miradi mipya na inayoendelea na utafiti katika maeneo ya TEHAMA, Kilimo, Afya, Viwanda na Maliasili. Aidha, Wizara itashirikiana na ofisi za Halmashauri ili kubaini wagunduzi na wabunifu ili kuboresha vipaji vyao. Vilevile, kituo cha kuendeleza ubunifu na ujasiriamali katika fani ya TEHAMA kitajengwa kwenye Taasisi ya Afrika ya Nelson Mandela ya Sayansi na Teknolojia pamoja

na kuanzisha Kituo mahiri cha “Agricultural Biotechnology” katika Chuo Kikuu cha Sokoine.

**Taasisi zinazohusika na Sayansi Teknolojia na Ubunifu**

**68.** **Mheshimiwa Spika,** naomba sasa nitumie fursa hii kueleza utekelezaji wa masuala ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu yaliyofanywa na Taasisi zetu za Sayansi na Teknolojia:

**Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH)**

**69.** **Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu kwa mwaka 2015/16 kupitia Tume ya Sayansi na Teknolojia, imefanya yafuatayo:

(i) imeratibu mtandao wa kuunganisha Vyuo Vikuu na Taasisi za Utafiti na Maendeleo ambapo taasisi **28** zimeunganishwa.

(ii) imeendelea kuhawilisha teknolojia mbalimbali nchini ambazo zimewezesha ujenzi wa maabara ndogo yenye uwezo wa kutoa machapisho mbalimbali kwa njia ya kidijitali kwa kutumia teknolojia ya *3D “printers”* ambazo zimetengenezwa hapa nchini kutokana na mabaki ya vifaa vingine vya kielektroniki. Ubunifu huu umefanyika katika Atamizi ya *BUNI* ambayo inasimamiwa na Tume.

(iii) imesimamia Kituo cha kuendeleza ubunifu (*BUNI Innovation Hub*) ambacho kimekuwa kikiendesha mpango maalum wa kuandaa waatamizi watarajiwa *(pre-incubation program)* kwa wanafunzi wa vyuo vikuu kupitia mafunzo kwa vitendo *(field practical and Internship program)*.

(iv) kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imeimarisha Atamizi ya TEHAMA *(ICT Incubator)* iliyopo katika Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Karume, na Atamizi ya Usarifu wa Mazao ya Kilimo *(Agribusiness Incubator)* iliyopo katika Kituo cha utafiti wa Kilimo cha Kizimbani, Zanzibar. Atamizi ya Usarifu wa mazao ya kilimo inalenga kuongeza mnyororo wa thamani katika kubiasharisha mazao mbalimbali ya kilimo na mifugo.

(v) Imetoa huduma za maktaba mtandao (e-library) na;

(vi) kutoa taarifa za utafiti kupitia tovuti ya utafiti (*Research web*).

**70.** **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/17 Wizara yangu kupitia Tume ya Sayansi na Tekonlojia itafanya yafuatayo:

(i) kuendelea kugharimia tafiti zenye kulenga kutatua matatizo ya wananchi;

(ii) kuanzisha mfumo wa kitaifa wa kufadhili tafiti za masomo baada ya Digrii ya uzamivu (post doctoral research);

(iii) kuanzisha mfumo wa kufuatilia viwango, ubora na maadili ya utafiti katika taasisi za utafiti na maendeleo;

(iv) kuhamasisha uanzishwaji wa atamizi katika vyuo vya elimu ya juu; na

(v) kujenga maabara ya kutunza maarifa na machapisho.

**Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam - (DIT)**

**71. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kutoa mafunzo ya teknolojia kwa wanafunzi na wafanyakazi wa viwandani ili waweze kujiongezea ujuzi mpya katika taaluma mbalimbali. Katika mwaka 2015/16 Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam, ilidahili wanafunzi wapya 1,386 ambapo 654 walikuwa ni Diploma ya Uhandisi, 648 Digrii ya Kwanza ya Uhandisi na 84 Digrii ya Uzamili ya Uhandisi na kufanya Taasisi kuwa na jumla ya wanafunzi 4,187 Wanawake 541 na wanaume 3,646. Aidha, Taasisi ilianzisha kozi mpya za Diploma ya Biotechnology, Digrii ya Uhandisi katika Mafuta na Gesi, Digrii ya Uzamili ya Matumizi ya

Teknolojia ya Ukokotoaji katika fani za Sayansi na Uhandisi na kupata ithibati kutoka NACTE.

72. **Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafunzo yaliyotajwa, Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam imejenga na kuendelea kuukarabati mtandao wa mawasiliano wa tiba mtandao (Telemedicine) unaounganisha hospitali 7 za Taifa Muhimbili, Rufaa Mbeya, Amana, Temeke, Mwananyamala, Tumbi Kibaha na Bagamoyo.

73. **Mheshimiwa Spika:** katika mwaka wa fedha 2016/17, Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam itatekeleza mambo yafuatayo:

(i) kuanzisha kozi mpya ya Diploma ya Uhandisi Ujenzi na Barabara (Civil and Highway Engineering);

(ii) kufundisha kozi mpya ya Digrii ya Uzamili katika Nishati Endelevu (MEng. Sustainable Energy);

(iii) kuendesha mafunzo ya awali (pre-entry) ili kupata wanafunzi wa kike 65 wasio na vigezo vya kutosha kudahiliwa katika kozi zinazoendeshwa na Taasisi;

(iv) kuendelea kuhudumia mradi wa matibabu mtandao (Telemedicine) kwa kushirikiana na Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto; na

(v) kuanza kufundisha kozi za Diploma za bidhaa za

ngozi (Leather goods) na Sayansi na Teknolojia ya Maabara (Science and Laboratory Technology) na kuendelea na utoaji wa kozi fupi na za kitaalam katika Teknolojia ya ngozi na bidhaa zake katika Kampasi ya Mwanza.

**Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Mbeya**

**74.** **Mheshimiwa Spika,** Chuo hiki kina majukumu ya kutoa mafunzo, kufanya utafiti na kutoa ushauri wa kitaalamu na kitaaluma. Katika mwaka 2015/16, *Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Mbeya* kilitekeleza yafuatayo:

(i) kudahili wanafunzi 3,682 ikiwa ni ongezeko la wanafunzi 82 kutoka kwa wanafunzi 3,600 waliodahiliwa mwaka 2014/15 ambayo ni sawa na ongezeko la asilimia 2;

(ii) kuajiri wafanyakazi katika fani mbalimbali (wafanyakazi 43 wameajiriwa kuanzia mwezi Julai 2015 mpaka Januari 2016);

**75.** **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/17 Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya kitaendelea kuongeza udahili wa wanafunzi kuhamasisha wanafunzi wa kike katika shule za sekondari kusoma masomo ya sayansi ili hatimaye waweze kujiunga na vyuo vya ufundi.

### Tume ya Nguvu za Atomiki

76. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2015/16 Wizara yangu kupitia Tume ya Nguvu za Atomiki imeendelea na jukumu lake la kudhibiti mionzi katika migodi na vituo vya huduma kwa kufanya yafuatayo: kukagua migodi 3 na vituo 72 kati ya vituo 100 sawa na asilimia 72 na kuhakikisha kuwa viwango vya mionzi vinavyotumika kwenye sehemu za kazi na vyakula vinadhibitiwa. Hili lilifanywa kwa kupima viwango vya mionzi kwa wafanyakazi 840 kutoka katika vituo 300 vya uzalishaji pamoja na kupima mionzi kwenye vyakula na mbolea kwa sampuli zipatazo 6,633.

77. **Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha kuwa vyanzo vya mionzi vinadhibitiwa na haviathiri mazingira na afya za viumbe hai, Wizara kupitia Tume ya Nguvu za Atomiki imesajili vyanzo vya mionzi vipatavyo 1045 na vituo vinavyomiliki vyanzo vya mionzi vipatavyo 1032. Kati ya vyanzo hivyo, 387 vina viasili vya mionzi *(radioactive materials).* Aidha, Tume pia kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imeweza kupima mionzi itokayo katika minara ya simu katika mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro, Dodoma, Arusha, Mwanza, Mbeya, Lindi na Mtwara. Vituo vipatavyo 294 vimepimwa na matokeo ya vipimo yameonesha viwango vya mionzi viko chini ya viwango vya usalama vya kimataifa.

78. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2016/17, Wizara yangu itaendelea na mikakati ya kuhakikisha kuwa wananchi na viumbe hai hawaathiriwi na mionzi hatarishi hasa kwenye sehemu za kazi kwa kufanya ukaguzi wa migodi 5 mikubwa inayofanya kazi ili kubaini hali ya usalama inayoendelea katika migodi hiyo. Aidha, vituo 120 vyenye vyanzo vya mionzi vitakaguliwa ili kubaini hali ya usalama kwa wafanyakazi 1,700 na umma kwa ujumla. Ukaguzi huu utasaidia kuandaa taratibu (*standard operating procedures*) za kufanya kazi katika maabara.

79. **Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu kupitia Tume ya Nguvu za Atomiki kwa mwaka 2016/17, itaendelea na udhibiti wa mionzi hatarishi kwa kusajili vituo vyenye vyanzo vya mionzi vipatavyo 1045 pamoja na kupokea na kutathimini maombi 450 ya leseni mbalimbali ili kuona kama yanakidhi matakwa ya Sheria na Kanuni za Usalama na Kinga ya Mionzi ya mwaka 2004. Aidha, Tume itakusanya mabaki ya mionzi katika vituo vyote na kuyahifadhi katika maabara maalum na kutafuta mabaki ya mionzi katika viwanda vinavyokusanya vyuma chakavu. Vile vile, Tume itaimarisha mfumo wa kielektroniki katika kutoa vibali, na kuwa na vifaa vya kupimia mionzi katika vituo 2, ambavyo ni Namanga na bandari ya Dar es salaam pamoja na kuanzisha vituo vya kanda ya kusini katika mikoa ya Ruvuma na Mbeya.

## 5.6 URATIBU WA TAASISI NA WAKALA

**80.** **Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu ina Taasisi na Wakala za elimu, Sayansi na Teknolojia inazozisimamia. Naomba sasa kutoa maelezo kuhusu Taasisi na Wakala hizo:

**Tume ya Taifa ya Vyuo Vikuu Tanzania**

**81.** **Mheshimiwa Spika,** Tume ya Vyuo Vikuu pia imefanya mapitio ya miongozo mbalimbali ya uthibiti ubora ili kuthibiti na kusimamia ithibati ya elimu ya juu nchini. Miongozo hiyo inajumuisha ya uhakiki ubora wa programu za masomo ya elimu ya juu na utoaji wa mafunzo katika ngazi ya Digrii za juu (postgraduate training). Miongozo hii imewezesha vyuo vya elimu ya juu kutoa elimu yenye viwango vinavyokidhi ubora kitaifa na kimataifa na mahitaji ya soko la ajira na jamii ya sasa na ya baadae.

**82.** **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2016/17, Wizara kupitia Tume ya Vyuo Vikuu imepanga kufanya yafuatayo**:**

(i) kusimamia ubora wa elimu ya Vyuo Vikuu vyote nchini kwa kufanya ukaguzi na tathmini za mara kwa mara vyuoni na pia mipango ya kuanzisha/kuhuisha Vyuo Vikuu 20 ili kusimamia ubora wa elimu itolewayo na Vyuo Vikuu nchini;

(ii) kuendelea kuratibu na kusimamia udahili wa wanafunzi wapatao 65,000 watakaojiunga na Vyuo Vikuu kupitia mfumo wa udahili wa pamoja (CAS), ili kufikia lengo la kuwa na wanafunzi wapatao 300,000 kwenye Taasisi za Elimu ya Juu nchini ifikapo mwaka 2017;

(iii) kuboresha mfumo wa ukusanyaji taarifa mbalimbali toka vyuo vya elimu ya juu nchini ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa sahihi kwa wakati zitakazosaidia katika kufikia maamuzi sahihi ya utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya elimu ya juu nchini;

(iv) kutathimini programu 200 za masomo katika Vyuo Vikuu nchini;

(v) kuendelea kuratibu na kuandaa Maonesho ya kumi na moja ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia ili kuelimisha umma kuhusu malengo, maendeleo na mchango wa Taasisi za Elimu ya Juu katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii nchini;

(vi) Kuendelea kuratibu mafunzo ya wanataaluma kutoka vyuo vikuu nchini wanaoendelea na masomo ya Uzamivu nchini Ujerumani (DAAD) kwa lengo la kukabiliana na changamoto za upungufu wa wanataaluma wenye sifa stahiki katika vyuo vikuu nchini; na

(vii) Kuanza ujenzi wa ofisi za kudumu za Tume katika kiwanja cha Uporoto, Dar es Salaam.

**Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (ADEM)**

83. **Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu una majukumu ya kuandaa na kuendesha mafunzo ya muda mfupi na mrefu katika uongozi na uendeshaji wa elimu; kufanya utafiti, kuandaa na kusambaza makala na vitabu pamojana kutoa ushauri wa kitaalamu katika mambo yanayohusu uongozi na uendeshaji wa elimu. Katika mwaka 2015/16, *Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu,* umefanya yafuatayo:

(i) umetoa mafunzo ya Uongozi na Usimamizi wa Elimu kwa ngazi ya Cheti kwa Walimu Wakuu 881 ambao wanaendelea na mafunzo katika Mikoa ya Mbeya, Njombe na Iringa; na ngazi ya Diploma ya Uongozi wa Elimu (DEMA) kwa walimu 815;

(ii) umetoa mafunzo ya Diploma ya Ukaguzi wa Shule kwa Wathibiti Ubora wa Shule 332 wa mwaka wa kwanza na 118 wa mwaka wa pili;

(iii) umekamilisha uanzishaji wa Kampasi ya Mbeya ambapo wanachuo 70 wameanza mafunzo ya Diploma ya Uongozi na Usimamizi wa Elimu (Diploma in Education Management and Administration);

(iv) umeendesha mafunzo ya Muda Mfupi ya Uongozi na Uendeshaji wa Elimu kwa Walimu

Wakuu 10,870 na Waratibu Elimu Kata 2,480, juu ya Uongozi wa Shule na Usimamizi wa Ufundishaji wa Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK);

(v) Maafisa Elimu Sekondari kutoka Halmashauri 179 wamepata mafunzo ya Uongozi wa Elimu na Udhibiti wa Majanga katika Elimu;

(vi) umefanya utafiti wa kubaini mahitaji ya mafunzo kwa walimu na wadau wengine kuhusu Uthibiti wa Ubora wa Elimu ili kuweza kuanzisha Digrii ya Menejimenti na Uthibiti wa Elimu (Bachelor in Education Management and Quality Assurance);

(vii) umetoa huduma ya Ushauri wa Kitaalamu juu ya Uongozi na Menejimenti ya Elimu kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, UNICEF, Rufiji Social Development Initiative, Equip(T) na SHIPO; na

(viii) umeandaa makala mbalimbali kwa wadau wake ambazo ni pamoja na Moduli ya Uongozi na Uthibiti wa Majanga kwa Maafisa Elimu Sekondari na Moduli ya Uongozi wa Shule na Usimamizi wa Ufundishaji KKK kwa Waratibu Elimu Kata na Walimu Wakuu.

**Uratibu wa Shughuli za UNESCO nchini**

**84. Mheshimiwa Spika,** Tume ya UNESCO ina majukumu ya kuratibu na kutekeleza programu za UNESCO nchini. Tume hii inatekeleza programu katika nyanja za Elimu, Sayansi Asilia, Sayansi Jamii, Utamaduni, Mawasiliano na Habari. Katika mwaka 2015/16, Tume ya Taifa ya UNESCO, ilifanya mapitio ya Toleo la 12 la Jarida la UNESCO Tanzania na kusambaza nakala 600 kwa wadau wa ndani na nje ya nchi kwa lengo la kutoa taarifa kuhusu shughuli zilizotekelezwa na Tume hiyo. Aidha, Tume imefanikiwa kuunganisha shule 10 za sekondari na chuo kimoja cha ualimu nchini kwenye mtandao wa shule nyingine duniani ili ziweze kubadilishana uzoefu wa kielimu kupitia mtandao wa shule wa *UNESCO Associated Schools Project Network* (ASP- Net).

**85. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka 2016/17 Wizara yangu kupitia *Tume ya Taifa ya UNESCO* itatekeleza yafuatayo:

(i) kutathmini miradi yote ya kielimu itakayopata ufadhili wa UNESCO makao makuu na ile itakayopata ufadhili kutoka kwa wafadhili wengine kupitia UNESCO;

(ii) kuendelea kutangaza na kuratibu ‘fellowships’ na ‘sponsorship’ zitakazoletwa nchini kwa lengo la kukuza weledi na uzoefu wa

wafanyakazi wa kada mbalimbali;

(iii) kuendelea na jitihada za kuunganisha Serikali ya Tanzania na UNESCO kupitia Wizara; na

(iv) kuendesha semina wezeshi zitakazojenga uwezo wa wadau katika kushiriki shughuli mbalimbali ikiwepo kuwa mstari wa mbele katika kutimiza malengo ya maendeleo ya dunia na maendeleo endelevu ifikapo 2030.

**Taasisi ya Elimu Tanzania**

**86.** **Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu inatambua umuhimu wa kuandaa mitaala bora ili elimu itolewayo iwe na viwango vinavyokubalika kitaifa na kimataifa. Wizara imekuwa ikitekeleza jukumu hili kupitia Taasisi ya Elimu Tanzania. Aidha, Taasisi hii inalo jukumu la kutoa miongozo kuhusu vifaa vya kufundishia na kujifunzia, kutoa mafunzo kwa walimu kazini na kufanya utafiti na ufuatiliaji wa utekelezaji wa mitaala katika ngazi za elimu ya Awali, Msingi, Sekondari na Ualimu.

**87.** **Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2015/16, Taasisi ya Elimu Tanzania imetekeleza yafuatayo:

(i) imeboresha Mtaala wa Elimu ya Awali na Elimu ya Msingi Darasa la III hadi VII ili uendane na dhana ya elimumsingi na kuandaa Mihtasari na Miongozo ya Elimu ya Awali na Elimumsingi

Darasa III – VI kwa masomo ya Kiswahili, English, Hisabati, Stadi za Kazi, Sayansi na Teknologia, Maarifa ya Jamii, Uraia na Maadili na Lugha ya Kifaransa;

(ii) imekusanya maoni ya wadau kuhusu mahitaji ya utekelezaji wa mtaala wa elimu ya sekondari Kidato cha 1-4 uliofanyika katika mikoa 26 ya Tanzania Bara ambapo Wilaya 52 na taasisi mbalimbali zilifikiwa;

(iii) imeandika na kusimamia uchapaji wa nakala 6,862,800 za vitabu 6 vya kiada kwa Darasa la Kwanza. Wizara imeweza kubaini kasoro za kiuchapaji kwenye nakala 2,807,600. Mchapaji amewajibishwa kurudia kazi hiyo kwa gharama zake;

(iv) imefanya tathmini ya vitabu vya ziada vilivyoandikwa na wachapishaji mbalimbali vitakavyotumika shuleni katika ngazi mbalimbali za elimumsingi, sekondari na vyuo vya ualimu ambapo jumla ya vitabu 146 vimefanyiwa tathmini kwa ajili ya kupewa ithibati; na

(v) imeandaa Mwongozo wa Walimu Washauri wa Vituo Shikizi (Satelite Schools) kwa ajili ya maandalizi ya shule za awali katika maeneo ambayo ni magumu kufikika.

88. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2016/17, Taasisi ya Elimu Tanzania imelenga kutekeleza yafuatayo:

(i) kutayarisha vitabu vya kiada vya Elimumsingi na sekondari vinavyozingatia mtaala ulioboreshwa;

(ii) kuhuisha na kuboresha mtaala wa elimu ya Msingi na Sekondari Kidato cha 1-4;

(iii) kuhuisha na kuboresha mtaala wa sekondari Kidato cha 5-6;

(iv) kuhuisha na kuboresha mtaala wa elimu ya ufundi; na

(v) kufanya tafiti za kielimu kuhusu mitaala inayotumika katika vyuo vya mafunzo ya elimu ya ualimu kwa lengo la kubaini ulinganifu wake na mitaala ya elimumsingi na sekondari.

**Baraza la Mitihani la Tanzania**

89. **Mheshimiwa Spika,** ili kusimamia upimaji na Utoaji Tuzo, Serikali kupitia Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA), liliendesha mitihani ya upimaji endelevu kwa watahiniwa 1,037,305 wa Darasa la Nne; na Kidato cha Pili watahiniwa 396,770; mitihani ya kumaliza Elimu ya Msingi kwa watahiniwa 763,606; na Kidato cha Nne watahiniwa 448,373 pamoja na upimaji wa Maarifa (QT) kwa watahiniwa 19,547.

**90.** **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2016/17 Baraza la Mitihani la Tanzania litaboresha mfumo wake wa ukusanyaji na uchakataji takwimu pamoja na kuweka mfumo wa kumtambua mwanafunzi kwa namba maalumu ili kuweza kufuatilia maendeleo ya mwanafunzi kuanzia anapoandikishwa mpaka anapomaliza mzunguko wa masomo. Baraza pia litaendelea kuimarisha utendaji wake kwa kusimika mashine mbili za kufunga bahasha zenye karatasi za mitihani (*Auto Poly Wrapping and Packing machines*) ili kuondokana na hatari na gharama za ufungaji wa mitihani kwa kutumia mikono na kuimarisha usalama wa Mitihani kwa kupunguza idadi ya watu wanaoshiriki katika maandalizi ya mitihani.

**Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA)**

**91.** **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ina majukumu ya kuratibu, kudhibiti, kugharimia, kutoa na kukuza mafunzo ya ufundi stadi nchini. Katika mwaka 2015/16, *Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi*, ilifanya yafuatayo:

(i) ilikamilisha taratibu za uandaaji wa Michoro ya ujenzi wa chuo cha Wilaya ya Karagwe pamoja na kuandaa Hadidu za Rejea (TOR) na ombi kwa ajili ya pendekezo (RFP) na kuwapatia washauri elekezi kwa ajili ya ujenzi

wa vyuo vya Wilaya za Chunya, Korogwe, Kilindi na Ukerewe.

(ii) iliendelea na ukarabati wa miundombinu ya vyuo vya ufundi stadi vya mikoa ya Tanga, Mwanza, Moshi, Kihonda (Morogoro) pamoja na chuo cha walimu wa ufundi stadi cha Morogoro.

(iii) imenunua mitambo na zana za kisasa za kufundishia na kujifunzia na zimeanza kutumika katika vyuo vya ufundi stadi vinne vya; Moshi-fani ya uchoraji majengo; Tanga- Vifaa vya fani ya Umeme wa majumbani na viwandani; Mwanza-fani ya TEHAMA na umeme; na Makete-vifaa vya fani ya ufundi magari.

(iv) ilitoa mafunzo kwa wanafunzi 400 waliopata mafunzo nje ya mfumo rasmi wa elimu na mafunzo (informal apprentices) katika Mikoa ya Mbeya na Dar es Salaam pamoja na kuwapatia mafunzo walimu wa ufundi 567 katika ngazi ya Cheti na Walimu 27 katika ngazi ya Diploma.

(v) ilitoa mafunzo ya kuwajengea uwezo watumishi 389 (wanaume 253 na wanawake 136) wanaofanya kazi katika Sekta Rasmi kwa makampuni 17 kupitia mpango unaojulikana kama ”Skills Enhancement Programme”.

(vi) ilitoa mafunzo katika vikundi mbalimbali vya sekta isiyo rasmi kwa washiriki wapatao 878

(Wanaume 344 wanawake 534) katika kutekeleza mpango wa mamlaka wa kuboresha na kuimarisha ufanisi wa utendaji kazi katika Seka isiyo rasmi.

**92.** **Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha kuwa mafunzo ya ufundi stadi yanatolewa katika kiwango cha ubora unaotakiwa na soko la ajira, tayari mamlaka imeimarisha eneo la ukaguzi kwa kuwajengea uwezo wakaguzi wapatao 66 (22 toka viwandani na 44 toka vyuoni) kwa mwaka huu wa fedha.

**93.** **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2016/17 Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi itatekeleza yafuatayo:

(i) kuendelea na ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi cha Mkoa wa Njombe na kuwapata Wakandarasi na kuanza ujenzi wa Vyuo vya Ufundi Stadi vya mikoa ya Geita, Simiyu na Rukwa;

(ii) kuanza ujenzi wa Vyuo vya Ufundi Stadi vya Wilaya za Namtumbo, Chunya, Kilindi na Ukerewe;

(iii) kukamilisha ukarabati wa miundombinu ya Vyuo vya Ufundi Stadi vya Tanga, Mwanza, Moshi, Kihonda na Chuo cha Mafunzo ya Ualimu wa Ufundi cha Morogoro;

(iv) kuanza ukarabati wa vyuo vya Wilaya ya

Karagwe na Korogwe;

(v) kusambaza vifaa vya kufundishia na kujifunzia katika Vyuo vya Ufundi stadi vya Iringa; Arusha Oljoro; Morogoro–Kihonda, Mkoa wa Mbeya; Mkoa wa Mwanza; na Chuo cha Ufundi stadi Singida pamoja na Chuo cha Walimu wa Ufundi Stadi cha Morogoro; na

(vi) Kuendelea kufanya tathmini na utahini kwa mafundi stadi wa nje ya mfumo rasmi wa mafunzo (informal apprentices) kwa kuongeza idadi ya fani na kuwajengea walimu wa ufundi stadi uwezo katika eneo hili.

**94.** **Mheshimiwa Spika**, pamoja na shughuli hizo Wizara yangu kupitia Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi itatekeleza yafuatayo:

(i) maandalizi ya awali kwa ajili ya kujenga vyuo vipya vya wilaya katika wilaya ya Chato na Nyasa;

(ii) ujenzi wa bweni la wasichana katika chuo cha VETA Makete;

(iii) ujenzi wa bweni la wasichana katika chuo cha VETA Mbeya;

(iv) kukamilisha ujenzi wa chuo cha ufundi stadi katika Halmashauri ya wilaya ya Busokelo na maandalizi ya kuanza mafunzo katika chuo hicho ifikapo 2017;

(v) ukarabati wa Chuo cha Ufundi Stadi cha katika Halmashauri ya wilaya ya Ruangwa; na

(vi) kuviwezesha vyuo viwili vya maendeleo ya Wananchi (Folk Development Colleges) vya Kibondo na Kasulu pamoja na Chuo kimoja cha Ufundi Stadi cha Nkowe ili kuimarisha mafunzo ya ufundi stadi.

**Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi**

95. **Mheshimiwa Spika,** kufuatia kuhamishiwa kwenye Wizara yangu Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi (FDC),Wizara imedhamiria kuvitumia Vyuo hivyo ili kuimarisha utoaji wa Mafunzo ya Ufundi stadi kwa maendeleo ya wananchi. Hivyo, katika mwaka wa fedha 2016/17, Wizara yangu imepanga kubainisha hali halisi ya miundombinu katika vyuo vyote vya FDC, na kuainisha Vyuo ambavyo vitaweza kutumika kutoa mafunzo ya Ufundi Stadi katika hali yake ya sasa kwa kuzingatia mahitaji ya jamii husika.

96. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2016/17, Wizara yangu kwa kutumia fedha zilizokuwa zimetengwa chini ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto itaanza ukarabati wa vyuo vya Ilula, Newala na Kilosa. Aidha, itajenga vyoo katika vyuo vya Buhangija, Bariadi na Kisarawe. Vilevile itaunganisha umeme katika vyuo vya Mwanhala,

Malya, Rubondo, Ulembwe, Munguri na Msingi. Wizara pia itashughulikia upatikanaji wa hatimiliki wa vyuo vya Kilwa Masoko, Chisalu, Kisarawe, Chilala, Arnautoglu, Musoma, Mwanva, Ikwiriri, Msingi na Ifakara.

**Mamlaka ya Elimu Tanzania**

**97.** **Mheshimiwa Spika**, katika kugharimia Elimumsingi hapa nchini, Serikali kupitia Mamlaka ya Elimu Tanzania inayosimamia mfuko wa Elimu nchini, imeweza kukusanya jumla ya Shilingi 33,647,048,003.00/= ambapo vyanzo vyake niTozo ya Elimu (Education Levy) kiasi cha Shilingi 30,486,481,326.00 na mapato ya ndani ni Shilingi 3,160,566,677.00.

**98.** **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2015/2016, Mamlaka ya Elimu Tanzania iliwezesha utekelezaji wa yafuatayo:

(i) Kuwajengea uwezo walimu na wanafunzi wa Hisabati, Biologia, Kingereza na Kiswahili ambapo walimu 15,000 na wanafunzi 6,000 walinufaika;

(ii) ilijenga mabweni 11 katika shule za Muyenzi (Ngara), Moyowasi (Kibondo), Mkongo (Rufiji), Endasak (Hanang), Shelui (Iramba), Kishamapanda (Busega), Kilumba (Nyasa), Mbuga (Mpwapwa), Kisiwani (Same), Kibaigwa

(Kongwa), na Ufana (Babati); na

(iii) Imegharimia uchapishaji wa vitabu 558,720 vya jinsi ya kujibu maswali ya mitihani ya Kidato cha Pili na cha Nne na Miongozo 75,360 katika kufanikisha mpango wa Matokeo Makubwa Sasa (BRN). Vitabu hivi vimewezesha walimu na wanafunzi kutambua mada ngumu na kutoa miongozo kwa walimu na watahiniwa kuhusu namna ya kujibu maswali ya mitihani hiyo.

**99.** **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2016/17, Mamlaka ya Elimu Tanzania itatekeleza yafuatayo:

(i) ukarabati wa majengo ya Shule kongwe 7 za Sekondari pamoja na kuzipatia vifaa vya maabara;

(ii) kuliwezesha Baraza la Mitihani kununua mitambo ya uchapishaji na ufungaji mitihani ili kuboresha na kufanikisha shughuli za uandaaji na utoaji wa mitihani; na

(iii) kutoa motisha kwa wanafunzi 10 watakaofanya vizuri na shule za msingi na sekondari 3000 zitakazofanya vizuri. Aidha, katika kupunguza changamoto za nyumba za walimu, Wizara itajenga nyumba za walimu 50 zitakazowezesha walimu 300 kupata makazi katika maeneo yasiyofikika kirahisi.

**Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu**

**100.** **Mheshimiwa Spika,** Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ni nyenzo kubwa katika kuongeza wataalam katika ngazi ya elimu ya juu nchini. Wizara kupitia Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, ilitoa Mikopo kwa wanafunzi wanaodahiliwa kusomea masomo ya kipaumbele kama vile Udaktari na Ualimu wa Sayansi na Hisabati. Mikopo hiyo pia imekua ikitolewa kwa wanafunzi wanaosomea fani adimu kama vile Uhandisi wa mafuta na gesi pamoja na Uhandisi umwagiliaji. Aidha, Serikali imeendelea kutoa mikopo kwa wanafunzi wanaosoma masomo mengine kwa kuzingatia viwango vya uhitaji.

**101.** **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2015/16 hadi kufikia Machi 2016, jumla ya wanafunzi 124,243 walikuwa wamepatiwa mikopo ya kiasi cha Shilingi 467,425,257,529.00. Idadi hii ilijumuisha wanafunzi 54,072 wa mwaka wa kwanza na 70,171 wanaoendelea na masomo. Aidha, Bodi pia ilitoa Mikopo kwa wanafunzi 7,996 wa Diploma ya Ualimu wa Hisabati na Sayansi na pamoja na wanafunzi 270 wa mafunzo ya sheria. Aidha, wanafunzi 685 wanaosomea nje ya nchi kwa makubaliano ya ushirikiano baina ya Tanzania na nchi rafiki (Algeria, Ujerumani, Cuba, Misri, Msumbiji, China na Urusi) hukopeshwa fedha za kujikimu.

102. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2016/17, wanafunzi 1,957 wanaosomea udaktari wa binadamu wamepatiwa ruzuku kwa kiasi cha Shilingi 5,514,656,888.00. Idadi hii inahusisha wanafunzi wanaoendelea na wanafunzi wapya kwenye fani hii ya udaktari wa binadamu.

**Mwongozo wa Utoaji Mikopo**

103. **Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu kupitia Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, imeboresha mwongozo wa utoaji mikopo kwa ajili ya mwaka 2016/17. Mwongozo huo unalenga kuondoa au kupunguza malalamiko kutoka kwa wanafunzi wasiopata mikopo kwa kuwapa kipaumbele waombaji wenye uhitaji mkubwa. Aidha, waombaji waliodahiliwa kwenye fani za vipaumbele vya kitaifa na masomo mengine watapatiwa mikopo kwa kuzingatia matokeo ya upimaji uwezo (Means Testing).

104. **Mheshimiwa Spika**, ili kuhakikisha kuwa wadau wa Bodi ya Mikopo wanapata taarifa sahihi na kupunguza malalamiko, katika mwaka 2016/17 Wizara yangu itaendelea kuendesha kampeni ya elimu kwa umma, ili kuelimisha wadau juu ya huduma zitolewazo na Bodi hiyo.

## Urejeshwaji Mikopo

105. **Mheshimiwa Spika**, kiwango cha urejeshwaji mikopo bado kipo katika kiwango kisichoridhisha. Changamoto zilizopo ni pamoja na kutokuwepo kwa mikakati thabiti ya ufuatiliaji wa wakopaji, udhaifu katika Sheria ya Bodi ya Mikopo ambapo, makato ya marejesho ya mikopo kutoka kwenye mshahara si ya lazima (*statutory deductions*). Aidha bado kuna mwitikio mdogo kutoka kwa wanufaika kujitokeza kuanza kurejesha mikopo yao pamoja na waajiri kutokutimiza majukumu yao ya kuwasilisha taarifa za wanufaika wa Mikopo.

106. **Mheshimiwa Spika,** ili kukabiliana na changamoto na kuongeza kasi ya marejesho ya mikopo katika mwaka 2016/17, Wizara yangu kupitia Bodi ya Mikopo imeweka mikakati ya kuongeza ukusanyaji na kasi ya marejesho ya mikopo kwa kushirikiana kwa karibu na mamlaka nyingine za Serikali kwenye kukusanya marejesho; na kuendelea kutoa elimu stahiki kwa wadau kuhusu urejeshwaji wa mikopo hii. Aidha Sheria ya Bodi ya Mikopo inafanyiwa marekebisho ili kuongeza kiwango cha urejeshwaji.

107. **Mheshimiwa Spika**, napenda kuchukua nafasi hii kuwakumbusha wanufaika wote wa mikopo kufanya marejesho ili watanzania wengine wenye uhitaji waweze kunufaika. Nawasihi wale wenye uwezo walipe kwa mkupuo mmoja ili kupunguza utegemezi

wa Bodi ya Mikopo kwa Serikali. Kwa kufanya hivyo, fedha zinazotengwa kwenye Bodi ya Mikopo zingeweza kutumika kuimarisha sekta ya elimu katika maeneo mengine muhimu. Aidha, napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza wale wote waliojitokeza kulipa mikopo yao kwa mkupuo mmoja.

## 5.7 USIMAMIZI WA UTEKELEZAJI WA PROGRAMU NA MIRADI

**108.** **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2015/16, Wizara yangu imeendelea kusimamia utekelezaji wa miradi na programu mbalimbali zinazotekelezwa katika ngazi zote za Elimu na Mafunzo.

### Programu ya Maendeleo ya Elimu ya Sekondari Awamu II (MMES II)

**109.** **Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu imeendelea kutekeleza Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES II) kwa ushirikiano na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa tangu mwaka 2010 hadi sasa. Mradi huu umelenga kuboresha miundombinu ya shule za sekondari 1,200; kuhakikisha kuwepo kwa walimu wa kutosha na kuboresha ufundishaji hususani katika masomo ya Hisabati, Sayansi na Lugha. Malengo mengine ni kusimamia matumizi sahihi ya rasilimali fedha kwenye shule kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia pamoja na kujenga uwezo

wa Wakala na Taasisi za Elimu ili kutekeleza mikakati ya kielimu iliyopo na ile ijayo.

110. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI imeimarisha mfumo wa takwimu kwa ajili ya kukusanya, kuchakata na kuhifadhi takwimu. Aidha, mfumo na zana zilizokuwa zinatumika katika ukusanyaji takwimu zimefanyiwa mapitio na kuboreshwa ili kukidhi mahitaji ya takwimu za elimu.

111. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2015/16, Wizara imetekeleza yafuatayo:

(i) imetoa mafunzo kwa walimu 3,419 wa shule za sekondari wa masomo ya Sayansi, Hisabati na Lugha; na

(ii) imefanya mapitio ya mwongozo wa mafunzo na moduli za ufundishaji na ujifunzaji kwa walimu wa masomo ya Sayansi, Hisabati na Lugha yenye lengo la kuhakikisha kuwa elimu bora yenye viwango vya kimataifa inatolewa kwa wanafunzi wa Kitanzania.

112. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2016/17, Wizara inalenga kutekeleza yafuatayo:

(i) kutoa mafunzo kwa walimu 7,000 wa masomo ya Sayansi, Hisabati na Lugha pamoja na kununua vifaa vya TEHAMA vya kufundishia na kujifunzia kwa Vituo 50 vya TEHAMA

vilivyopo kwenye Shule za Sekondari;

(ii) kufanya ufuatiliaji na tathmini ya miundombinu ya shule za sekondari 408 itakayojengwa kupitia Halmashauri mbalimbali nchini;

(iii) kufanya tathmini ya MMES II na kuandaa Andiko la Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari Awamu ya Tatu (MMES III);

(iv) kukagua matumizi ya fedha za MMES II kwenye Wizara na Halmashauri;

(v) kugharimia uchapaji wa vitabu vya Sayansi na Hisabati; na Kiongozi cha Mwalimu kwa wanafunzi wasioona na wenye uono hafifu;

(vi) kuhakiki uchakataji na uboreshaji wa mfumo wa ukusanyaji takwimu za elimu na kutegemeza matumizi ya takwimu; na

(vii) kuwezesha na kutegemeza shughuli za MMES II zinazohusiana na mpango wa Matokeo Makubwa Sasa (BRN).

**Mradi wa Kusaidia Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (Literacy and Numeracy Education Support (LANES)**

**113. Mheshimiwa Spika,** katika juhudi za kuhakikisha kwamba watoto wanaojiunga na elimu ya msingi wanamudu vema stadi za Kusoma Kuandika na Kuhesabu, Wizara yangu inaendelea na uratibu wa

utekelezaji wa Programu wa Kukuza Stadi za KKK.

114. **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa fedha 2015/16, Wizara imetekeleza yafuatayo:

(i) imegharimia mapitio ya Mitaala ya Elimu ya Awali na Msingi kwa lengo la kwenda sambamba na dhana ya Elimumsingi;

(ii) imegharimia mafunzo kuhusu mabadiliko ya ufundishaji na ujifunzaji wa Stadi za KKK kwa Wathibiti Ubora wa Shule 1,500. Aidha, magari 38 yamenunuliwa na kugawiwa katika Wilaya ambazo hazikuwa na magari na hivyo kuwawezesha Wathibiti Ubora wa Shule kuzifikia shule nyingi zaidi na kwa urahisi; na

(iii) imegharimia mafunzo ya menejimenti na uongozi wa shule kwa Waratibu Elimu Kata 2,480 na Walimu wakuu wa Shule za Msingi 10,870. Kupitia mafunzo haya Walimu Wakuu wa shule za msingi sasa wataweza kuandaa na kutekeleza Mipango ya Maendeleo ya Shule kwa ufanisi zaidi (*Whole School Development Plan*).

115. **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa fedha 2016/17, Wizara yangu kupitia programu hii itatekeleza yafuatayo:

(i) itaimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa stadi

za KKK kwa kutoa mafunzo kabilishi kwa walimu 22,955 wa Darasa la III & IV kuhusiana na mtaala uliohuishwa;

(ii) itakamilisha mpango wa kuimarisha miundombinu ya matumizi ya mfumo wa kielektroniki kwenye Halmashauri zote nchini. Mfumo huu utasaidia upatikanaji wa takwimu za ngazi ya shule moja kwa moja kwenye mtandao na hivyo kupunguza kwa kiasi kikubwa gharama za ukusanyaji wa takwimu kwenye mifumo isiyo ya kisasa;

(iii) itagharimia usimikaji mfumo wa kielektroniki wa ukusanyaji taarifa za wanafunzi chini ya Baraza la Mitihani Tanzania ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa hizo wakati wa Mitihani. Utaratibu huu utaisaidia Serikali kupunguza matumizi makubwa ya fedha za ukusanyaji taarifa chini ya mfumo wa TSM9;

(iv) itawezesha kamati za shule kupata mafunzo ya kuandaa mipango ya maendeleo ya shule kwa lengo la kuziwezesha kutekeleza majukumu yake kwa ukamilifu ili kuharakisha maendeleo ya shule;

(v) itahamasisha jamii kushiriki kwenye utekelezaji wa mpango wa LANES kupitia vyombo vya habari na utoaji taarifa kwa umma, machapisho, matamasha na vikundi vya watoto (childrens 3Rs Clubs);

(vi) kutoa nafasi za masomo na tafiti ili kuongeza ufahamu wa masuala ya elimu ya awali;

(vii) kuajiri mtaalamu elekezi kuandaa na kutekeleza katika ngazi ya majaribio maudhui ya kieletroniki ya KKK ili yatumike kuongeza ari ya kujifunza kwa watoto;

(viii) kufanya tathmini ya Sekta ya Elimu na kutumia mapendekezo yake kutengeneza Mpango wa Maendeleo wa Elimu wa miaka mitano 2016/17 hadi 2020/21;

(ix) kufuatilia na kutathmini mipango ya Sekta ya Elimu; na

(x) kuimarisha usimamizi, utekelezaji na ufuatiliaji wa mipango ya LANES kwa kutoa mafunzo ya matumizi bora ya rasilimali fedha kwa Watendaji na Wakurugenzi pamoja na kununua vifaa vya uendeshaji kwa Idara, Taasisi na vitengo vinavyotekeleza LANES.

**Mradi wa Huduma ya Maji, Elimu ya Afya na Usafi wa Mazingira Shuleni “School Water, Sanitation and Hygiene (SWASH)”**

**116.** **Mheshimiwa Spika**, lengo la Mradi wa Huduma ya Maji, Afya na Usafi wa Mazingira ni kuboresha miundombinu ya vyoo bora, upatikanaji wa maji safi na salama pamoja na utoaji wa elimu ya afya na kutunza mazingira ya shule. Katika mwaka

2015/16, miundombinu ya vyoo vya shule za msingi 1,087 iliboreshwa; shule 2,531 ziliunda vikundi vya usafi ambavyo hutoa elimu ya afya shuleni; na kuweka vifaa vya kunawia mikono shuleni. Aidha, timu za usafi wa mazingira za mikoa 10 (Dar es Salaam, Morogoro, Ruvuma, Njombe, Iringa, Tanga, Kilimanjaro, Pwani, Dodoma na Mtwara) ya Tanzania Bara zilipatiwa elimu elekezi kuhusu utumiaji wa Mwongozo wa Huduma ya Maji, Elimu ya Afya na Usafi wa Mazingira shuleni.

**117.** **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/17, mradi wa SWASH umelenga kufikia jumla ya shule 4,200 (za msingi 3,500 na 700 za sekondari). Aidha, Serikali itashirikisha wadau mbalimbali wa elimu ili kupata rasilimali fedha ili kutatua tatizo la ukosefu wa vyoo bora shuleni.

**118.** **Mheshimiwa Spika,** mradi huu pia umelenga kutekeleza yafuatayo:

(i) kufanya ufuatiliaji na tathmini ya ujenzi wa vyoo bora kwenye shule zilizopatiwa fedha za mradi, kujenga uwezo wa utekelezaji na upanuzi wa mradi kwa waratibu wa mradi ngazi ya Mkoa na Halmashauri na kuwezesha kuandaa mfumo wa ukusanyaji takwimu za taarifa za upatikanaji maji, vyoo bora na vifaa vya unawaji mikono;

(ii) kukusanya takwimu za vyoo, maji na elimu ya usafi wa mazingira shuleni ili kupanga mipango ya muda mfupi na mrefu ya kuboresha miundombinu ya vyoo na mifumo ya maji katika mikoa 14; na

(iii) kufanya mapitio ya Mpango Mkakati wa huduma ya maji, afya na usafi wa mazingira, kuchapa miongozo, kugharimia ununuzi wa vitendea kazi na kuendesha harambee kwa ajili ya ujenzi wa vyoo na miundombinu ya maji safi na taka.

**Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu (Mpango wa Ugharimiaji - Lipa Kulingana na Matokeo (Programme for Results – P4R)**

**119.** **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kutekeleza programu mpya ya kufadhili sekta ya elimu inayoitwa "Lipa Kulingana na Matokeo" (P4R) kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo ambao ni Benki ya Dunia, DfID na Sida. Programu hii inalenga kujenga uwezo wa Serikali wa kutekeleza vipaumbele vyake ilivyojiwekea. Programu ilianza kutekelezwa mwaka 2014/15 ambapo mpaka sasa jumla ya Shilingi bilioni 90 zimepatikana kutokana na Serikali kutekeleza vipaumbele vyake kwa ufanisi. Aidha, kupitia programu hii, Wizara imelenga kuhakikisha madai yote ya walimu yasiyo ya mishahara yanalipwa. Kupitia programu hii, hadi kufikia mwezi Aprili, 2016 jumla ya walimu 63,409 wa shule za

msingi na sekondari wameshalipwa madai yao yanayofikia Shilingi bilioni 22.24.

**120. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2016/17, Wizara yangu itatumia fedha zitakazopatikana kupitia programu hii kusaidia kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa kufanya ukarabati mkubwa kwa shule kongwe za sekondari nchini. Kwa hivi sasa uchambuzi wa mahitaji ya ukarabati (conditional survey) wa shule 22 za awamu ya kwanza unafanyika na ukarabati unategemewa kuanza mwezi Agosti, 2016.

**121. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2016/17 Serikali imejipanga kuhakikisha kuwa shule zetu za sekondari zina vifaa vya maabara na vitabu vya kutosha ambapo tayari Wizara yangu imetangaza zabuni ya ununuzi wa vifaa hivyo vya maabara na uchapaji wa vitabu hivyo, ambavyo vitasambazwa nchini kote. Maabara zote zilizojengwa na Halmashauri kwa kushirikiana na wananchi zitapatiwa vifaa vya maabara. Ununuzi wa vifaa vya maabara utafanyika kwa awamu tatu ambapo awamu ya mwisho inategemewa kukamilika mwaka wa fedha 2018/19. Nia ya Serikali katika mpango huu ni kuhakikisha kuwa elimu inayotolewa inakidhi viwango na wanafunzi wanapatiwa zana zote muhimu katika kujifunza.

**122. Mheshimiwa Spika,** nitumie fursa hii kuzihamasisha Halmashauri ambazo hazijakamilisha maabara zikamilishe ili ziweze kunufaika na mpango huu wa Wizara yangu wa kutoa vifaa vya maabara.

**Mradi wa Kutegemeza Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi na Elimu ya Ualimu**

**123. Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu inatekeleza mradi wa kutegemeza Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi na Elimu ya Ualimu unaolenga kuongeza udahili, usawa na ubora katika maeneo hayo. Hii inahusisha pia kujenga uwezo wa wakufunzi na walimu wa sekondari na vyuo vya Ualimu katika masomo ya Sayansi na Hisabati. Katika mwaka wa fedha 2015/16 mradi umefadhili walimu 5 wa Chuo cha Ufundi Arusha, watatu katika ngazi ya Digrii ya uzamili na wawili katika ngazi ya uzamivu. Aidha, wanataaluma 162 wa vyuo vya ufundi vilivyosajiliwa na NACTE wamejengewa uwezo katika kuendeleza mitaala, kufundisha na kutathmini mafunzo yanayozingatia umahiri ili kuinua ubora wa Elimu na Mafunzo yatolewayo katika Vyuo vya Ufundi.

**124. Mheshimiwa Spika,** mradi huu umewezesha ununuzi wa kompyuta 400 kwa ajili ya vyuo 40 vya ufundi. Aidha, katika mwaka 2016/17 mradi unalenga kukarabati vyuo sita vya ualimu wa

Sayansi vya Dakawa, Tabora, Kleruu, Butimba, Mpwapwa na Marangu ambapo kwa mwaka 2015/2016 uchambuzi wa awali wa mahitaji ya ukarabati umefanyika. Vilevile, mradi utagharimia ukarabati wa Chuo cha Ualimu wa Ufundi Stadi cha Morogoro na kununua vifaa vya maabara kwa ajili ya mafunzo ya ufundi kwenye fani za gesi na mafuta kwa Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi cha Mkoa wa Mtwara.

125. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2016/17, mradi huu utawezesha ununuzi wa vifaa mbalimbali vya kufundishia na kujifunzia katika vyuo vya Ufundi Stadi vya Mikoa ya Mtwara, Njombe, Geita, Simiyu na Rukwa ili kuinua ubora wa Elimu na Mafunzo yatolewayo katika Vyuo vya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi. Aidha, mradi pia utaanza ujenzi na ukarabati wa majengo ya hosteli na madarasa katika Chuo cha Ualimu wa Ufundi Stadi Morogoro.

**Mradi wa Ukarabati na Upanuzi wa Vyuo vya Ualimu vya Ndala, Shinyanga, Kitangali na Mpuguso (Upgrading of Teachers' Colleges)**

126. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/17, Wizara yangu itatekeleza Mradi wa Ukarabati na Upanuzi wa Vyuo vya Ualimu vya Shinyanga, Mpuguso, Ndala na Kitangali ambao unalenga kuinua ubora wa elimu ya msingi na sekondari. Lengo la mradi

huu ni kuboresha mazingira ya kusomea kwa walimu waliopo, kusaidia kuvutia walimu wapya na kuhakikisha kuwa walimu wanafunzi wana motisha ya kupata ujuzi ili waweze kutoa elimu bora kwa wanafunzi wao mara watakapohitimu. Idadi ya watakaohitimu baada ya kukamilika kwa ukarabati wa vyuo hivi vinne inatarajiwa kufikia wanachuo 3,300 kwa mwaka.

**Mradi wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu (STHEP)**

**127.** **Mheshimiwa Spika**, katika kuimarisha miundombinu na ufundishaji wa Elimu ya Juu, Wizara imetekeleza Mradi wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu kwa Awamu ya Pili, kuanzia mwezi Septemba 2014 hadi Januari 2016. Mradi huu umepata ufadhili wa Benki ya Dunia. Vyuo na Taasisi za Elimu ya Juu zilizonufaika katika mradi huu ni;

(i) Chuo Kikuu cha Dar es Salaam,
(ii) Chuo Kikuu cha Ardhi,
(iii) Chuo Kikuu Huria cha Tanzania,
(iv) Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo,
(v) Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar,
(vi) Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu cha Dar es Salaam,
(vii) Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa,
(viii) Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam,
(ix) Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu,
(x) Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi; na
(xi) Tume ya Vyuo Vikuu.

**128. Mheshimiwa Spika,** malengo ya mradi huu yalikuwa ni kujenga uwezo wa wanataaluma na watumishi wa Vyuo Vikuu na Taasisi za Elimu ya Juu kwa kudhamini mafunzo katika ngazi ya uzamili na uzamivu, kujenga miundombinu mipya ya vyuo vikuu na kufanya ukarabati wa majengo katika Taasisi. Mradi pia ulisaidia ununuzi wa vifaa na samani za kufundishia na kujifunzia kulingana na vipaumbele vya Taasisi husika.

**129. Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia mwezi Aprili, 2016 mradi umegharimia masomo ya wanataaluma 188 wa ngazi ya uzamivu (asilimia 30 ni wanawake); na wanataaluma 208 wa ngazi ya uzamili (asilimia 28 ni wanawake). Zaidi ya asilimia 60 ya wanufaika wamehitimu mafunzo yao na wanaendelea na kazi katika Taasisi zao na waliobaki wako katika hatua za mwisho za kuhitimisha mafunzo yao.

**130. Mheshimiwa Spika,** mradi pia umejenga majengo mapya 25 ya kufundishia na kujifunzia, na pia umefanyia ukarabati majengo yaliyokuwepo katika vyuo vikuu 7**.** Ujenzi na Ukarabati huo umeviongezea vyuo vikuu uwezo wa kuchukua wanafunzi wa elimu ya juu 47,622 zaidi ikilinganishwa na kabla ya mradi. Aidha, wakutubi, wataalamu wa maabara na watumishi wengine 1,794 katika taasisi za ARU, DUCE, DIT, OUT, MUCE, SUA, na UDSM walipata mafunzo ya muda mfupi ya kuwaongezea ujuzi katika maeneo yao. Vile vile wananchi 2,194

wanaozunguka vyuo wamenufaika na miundombinu ya kitafiti iliyojengwa kama vile mitambo ya kusafisha maji taka iliyojengwa Chuo Kikuu cha Ardhi, Dar es Salaam.

131. **Mheshimiwa Spika,** mradi pia umewezesha ununuzi wa vifaa vya maabara 5,634 vinavyotumiwa na wanafunzi 16,600 wa elimu ya juu**.** Kwa upande wa TEHAMA vifaa 1,831 vilivyonunuliwa vimeweza kusaidia wanafunzi takriban 5,400 katika fani mbalimbali za elimu ya juu. Aidha, vitabu 6,121 vilisambazwa kwenye Taasisi na vilipunguza tatizo la upungufu wa vitabu kwa kiasi kikubwa. Hatua hizi zimechochea ongezeko na ubora wa wanafunzi wanaohitimu katika fani ya Sayansi na Teknolojia kutoka wahitimu 3,353 kwa mwaka 2007 hadi kufikia wanafunzi zaidi ya 8,294 mwaka 2015.

132. **Mheshimiwa Spika,** mradi pia umewezesha ujenzi wa mfumo wa kielektroniki kwa ajili ya udahili wa wanafunzi wa Elimu ya Juu nchini. Mfumo huu umewezesha waombaji kuchagua programu katika vyuo mbalimbali kwa ufanisi kupitia mtandao na simu za mkononi. Aidha, mfumo huu umesaidia kuondoa tatizo la wanafunzi kudahiliwa katika chuo zaidi ya kimoja pamoja na kubaini wanaotumia matokeo ya kughushi kwa kuwa mfumo huu umeunganishwa na Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA). Mfumo huu umepunguza kwa kiasi kikubwa gharama za maombi ya udahili katika vyuo

vya elimu ya juu kwa kuwa mwombaji anaomba na kulipia mara moja tu.

**Mradi wa Elimu na Kukuza Stadi za Kazi na Ujuzi (Education and Skills for Productive Jobs Program– ESPJ)**

**133. Mheshimiwa Spika**, baada ya kukamilisha mradi wa Sayansi, Teknolojia na Ubunifu, Wizara imeandaa mradi mpya utakaoanza mwaka 2016/17 kwa ajili ya kukuza stadi za kazi na ujuzi. Mradi huu umeandaliwa ili kuwezesha utekelezaji wa Mkakati wa Kitaifa wa Kukuza na kupanua stadi za kazi na ujuzi. Mkakati huu uliandaliwa na Wizara yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi Vijana na Ajira, na Walemavu. Mradi utajikita katika kuongeza fursa za upatikanaji wa stadi za kazi na kuongeza ujuzi katika sekta sita za kipaumbele za kukuza uchumi ambazo ni kilimo na kilimo uchumi, utalii, uchukuzi, ujenzi, nishati na madini; na TEHAMA. Uchaguzi wa sekta hizi umezingatia mahitaji makubwa ya waajiri katika sekta hizo, mchango wa sekta katika uchumi, upungufu mkubwa wa wataalamu, uwezo wa kuongeza ajira; na mahusiano kati ya sekta hizi na nyingine.

134. **Mheshimiwa Spika**, lengo kuu la mradi wa ESPJ ni kuimarisha na kupanua upatikanaji na ukuzaji wa ubora wa stadi za kazi na ujuzi katika ngazi za ufundi na ufundi stadi, elimu ya juu na sekta isiyo rasmi kwenye maeneo lengwa. Aidha, mradi unalenga kuimarisha mfumo wa kitaasisi wa kusimamia, kuratibu na kugharimia uendelezaji stadi za kazi katika ngazi ya kitaifa na kisekta kwa kushirikiana na sekta binafsi. Jumla ya wanafunzi watakaopata mafunzo katika mradi inatarajiwa kuwa zaidi ya 47,000 kwa miaka mitano. Mradi huu wa miaka mitano kuanzia mwaka 2016/17 unagharimiwa na Serikali kupitia mkopo wa Dola za Kimarekani milioni 120 kutoka Benki ya Dunia.

## 6.0 SHUKRANI

135. **Mheshimiwa Spika,** napenda kutambua mchango mkubwa wa viongozi wenzangu katika Wizara. Kwa namna ya pekee namshukuru sana Mheshimiwa Mhandisi Stella Martin Manyanya (Mb) Naibu Waziri, kwa ushirikiano mkubwa anaonipa. Aidha, namshukuru Katibu Mkuu, Bi. Maimuna Kibenga Tarishi; Manaibu Makatibu Wakuu; Profesa Simon Samwel Msanjila na Dkt. Leonard Douglas Akwilapo, Kamishna wa Elimu, Wakurugenzi, Wakuu wa Vitengo na Wakuu wa Taasisi mbalimbali zilizo chini ya Wizara yangu kwa ushirikiano wao katika kutekeleza majukumu yetu ya kila siku. Napenda pia kuwashukuru, Viongozi wa Vyama vya Wafanyakazi, Watumishi wa Wizara, Wanataaluma, Wanafunzi na wadau wote wa Elimu kwa ushirikiano wao katika kuendeleza Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi.

136. **Mheshimiwa Spika**, napenda kuwashukuru wadau wote wa sekta ya elimu, sayansi, teknolojia na ufundi wakiwemo Washirika wa Maendeleo, viongozi mbalimbali na kwa namna ya pekee wananchi ambao wamechangia sana katika kufanikisha utekelezaji wa mipango ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi.

137. **Mheshimiwa Spika**, washirika mbalimbali wa Maendeleo na wadau wa Elimu wamechangia katika kufanikisha mipango ya Elimu, Sayansi, Teknolojia

na Ufundi kwa kuwa si rahisi kuwataja wote. Napenda kuchukua fursa hii kwa niaba ya Wizara yangu, kuwashukuru na kuwatambua baadhi yao kama ifuatavyo: Serikali za Algeria, Canada, China, Cuba, India, Italia, Japan, Urusi, Denmark, Finland, Norway, Marekani, Mauritius, Msumbiji, Misri, Norway, Sweden, Uingereza, Ujerumani, Korea Kusini, Uturuki na Jumuiya ya Afrika Mashariki.

**138.** **Mheshimiwa Spika**, napenda pia kuyashukuru mashirika yaliyochangia katika kufanikisha programu za Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi ambayo pamoja na: Aga Khan Education Services, Airtel, Barclays Bank, Benki Kuu, Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, Benki ya Taifa ya Biashara, British Council, Campaign for Female Education (CAMFED), Care International, Children International, Children's Book Project, Commonwealth Secretariat, Benki ya CRDB, DAAD, DfID, Education Quality Improvement Programme (EQUIP(T)), FEMINA, Ford Foundation, GIZ, Global Partnership for Education, International Labour Organisation (ILO), International Reading Association, Irish Aid, Inter University Council of East Africa (IUCEA), Japan International Cooporation Agency (JICA), Korea International Cooporation Agency (KOICA), National Micro Finance Bank (NMB), Peace Corps, Plan International, Rockefeller, Swedish International Development Agency (Sida), Sight Savers

International, Tanzania Education Network / Mtandao wa Elimu Tanzania (TENMET), Tigo, Umoja wa Nchi za Ulaya, United Nations Development Programme (UNDP) , UNESCO, UNICEF na WaterAid.

## 7.0 MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2016/17

139. **Mheshimiwa Spika**, ili kuwezesha utekelezaji wa malengo yaliyopangwa katika mwaka 2016/17, Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi inaomba kuidhinishiwa jumla ya Shilingi **1,396,929,798,625.00** ili kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

140. **Mheshimiwa Spika**, katika maombi haya:

(i) Shilingi **499,272,251,000.00** zinaombwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ya Wizara ambapo Shilingi **386,904,995,000.00** ni kwa ajili ya mishahara na Shilingi **112,367,256,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo;

(ii) Shilingi **84,132,297,000.00** zinaombwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ya Idara na Vitengo. Kati ya hizo, Shilingi **57,246,945,000.00** ni kwa ajili ya mishahara, na Shilingi **26,885,352,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo;

(iii) Shilingi **415,139,954,000.00** zinaombwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ya Taasisi. Kati ya hizo, Shilingi **329,658,050,000.00** ni kwa ajili ya mishahara, na Shilingi **85,481,904,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo; na

(iv) Shilingi **897,657,547,625.00** zinaombwa kwa

ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya hizo, Shilingi **620,693,856,575.00** ni fedha za ndani na Shilingi **276,963,691,050.00** ni fedha kutoka kwa washirika wa maendeleo.

**141. Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Wizara yangu, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwako binafsi na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Hotuba hii inapatikana pia katika tovuti ya Wizara kwa anwani ya: http://www.moe. go.tz.

**142. Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

## VIAMBATISHO

### Kiambatisho Na.1: Udahili kwa Vyuo vya Elimu ya Juu vya Umma - Mwaka wa Masomo 2015/16

| Na. | Taasisi | Ke | Me | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Ardhi University | 407 | 722 | 1129 |
| 2 | Arusha Technical College | 13 | 69 | 82 |
| 3 | Center for Foreign Relations Dar es Salaam | 85 | 106 | 191 |
| 4 | College of African Wildlife Management Mweka | 49 | 135 | 184 |
| 5 | College of Business Education | 497 | 610 | 1107 |
| 6 | Community Development Training Institute | 146 | 102 | 248 |
| 7 | Dar es Salaam Institute of Technology | 112 | 579 | 691 |
| 8 | Dar Es Salaam Maritime Institute | 7 | 85 | 92 |
| 9 | Dar es Salaam University College of Education | 527 | 1441 | 1968 |
| 10 | Eastern Africa Statistical Training Centre | 22 | 63 | 85 |
| 11 | Institute of Accountancy Arusha | 346 | 399 | 745 |
| 12 | Institute of Adult Education | 157 | 147 | 304 |

| Na. | Taasisi | Ke | Me | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| 13 | Institute of Finance Management | 1002 | 1629 | 2631 |
| 14 | Institute of Rural Development Planning | 255 | 385 | 640 |
| 15 | Institute of Social Work | 432 | 227 | 659 |
| 16 | Institute of Tax Administration | 30 | 99 | 129 |
| 17 | Mbeya University of Science and Technology | 124 | 929 | 1053 |
| 18 | Mkwawa University College of Education | 337 | 1179 | 1516 |
| 19 | Moshi Cooperative University | 479 | 602 | 1081 |
| 20 | Muhimbili University of Health and Allied Sciences | 187 | 418 | 605 |
| 21 | Mzumbe University | 1542 | 1668 | 3210 |
| 22 | National Institute of Transport | 455 | 1529 | 1984 |
| 23 | Open University of Tanzania | 193 | 441 | 634 |
| 24 | Sokoine University of Agriculture | 703 | 1838 | 2541 |
| 25 | State University of Zanzibar | 469 | 348 | 817 |
| 26 | Tanzania Institute of Accountancy | 1293 | 1387 | 2680 |
| 27 | The Mwalimu Nyerere Memorial Academy DSM | 403 | 534 | 937 |
| 28 | University of Dar es Salaam | 1884 | 3792 | 5676 |
| 29 | University of Dodoma | 2252 | 5702 | 7954 |

| Na. | Taasisi | Ke | Me | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| 30 | Water Development Management Institute | 37 | 174 | 211 |
| 31 | Zanzibar Institute of Financial Administration | 71 | 72 | 143 |
| **Jumla** | | **14,516** | **27,411** | **41,927** |

**Kiambatisho Na.2: Udahili kwa Vyuo vya Elimu ya Juu vya Binafsi - Mwaka wa Masomo 2015/16**

| Na. | Taasisi | Ke | Me | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Aga Khan University | 25 | 3 | 28 |
| 2 | Algerian Scholarships | 8 | 44 | 52 |
| 3 | Archbishop James University College | 161 | 524 | 685 |
| 4 | Archbishop Mihayo University College of Tabora | 121 | 291 | 412 |
| 5 | AbdulRahman Al-Sumit Memorial University | 154 | 111 | 265 |
| 6 | Catholic University of Health and Allied Sciences | 211 | 294 | 505 |
| 7 | Centre for Development Cooperation (Arusha) | 1 | 1 | 2 |
| 8 | Eckernforde Tanga University | 26 | 43 | 69 |
| 9 | Hubert Kairuki Memorial University | 138 | 136 | 274 |
| 10 | Institute of Procurement and supply | 7 | 8 | 15 |
| 11 | International Medical and Technological University | 98 | 223 | 321 |

| Na. | **Taasisi** | **Ke** | **Me** | **Jumla** |
|---|---|---|---|---|
| 12 | Jomo Kenyatta University of Agriculture and Technology | 8 | 7 | 15 |
| 13 | Jordan University College | 293 | 431 | 724 |
| 14 | Josiah Kibira University College | 61 | 286 | 347 |
| 15 | Kampala International University Dar es Salaam Conventional | 382 | 783 | 1165 |
| 16 | Kilimanjaro Christian Medical College | 248 | 383 | 631 |
| 17 | Marian University College | 92 | 282 | 374 |
| 18 | Mount Meru University | 76 | 136 | 212 |
| 19 | Mount Meru University(Mwanza Centre) | 27 | 49 | 76 |
| 20 | Mozambique Scholarships | 11 | 36 | 47 |
| 21 | Muslim University of Morogoro | 273 | 681 | 954 |
| 22 | Mwenge Catholic University | 315 | 848 | 1163 |
| 23 | Ruaha Catholic University | 241 | 656 | 897 |
| 24 | Sebastian Kolowa Memorial University | 179 | 412 | 591 |
| 25 | St Johns University of Tanzania (Msalato Centre) | 1 | 2 | 3 |
| 26 | St Johns University of Tanzania (St. Mark’s Centre) | 29 | 30 | 59 |
| 27 | St. Augustine University in Tanzania Mbeya Center | 113 | 265 | 378 |
| 28 | St. Augustine University of Tanzania | 640 | 1218 | 1858 |
| 29 | St. Augustine University of Tanzania(Arusha Centre) | 108 | 209 | 317 |
| 30 | St. Augustine University of Tanzania(Bukoba Centre) | 29 | 101 | 130 |

| Na. | **Taasisi** | **Ke** | **Me** | **Jumla** |
|---|---|---|---|---|
| 31 | St. Francis University College of Health and Allied Sciences | 70 | 162 | 232 |
| 32 | St. Johns University of Tanzania | 529 | 880 | 1409 |
| 33 | St. Joseph University College of Agricultural Sciences and Technology | 125 | 355 | 480 |
| 34 | St. Joseph University College of Health and Allied Sciences | 173 | 307 | 480 |
| 35 | St. Joseph University College of Management and Commerce | 1 | | 1 |
| 36 | Stefano Moshi Memorial University College | 85 | 116 | 201 |
| 37 | Stella Maris Mtwara University College | 124 | 140 | 264 |
| 38 | Teofilo Kisanji University | 190 | 451 | 641 |
| 39 | Teofilo Kisanji University Dar es Salaam College | 68 | 46 | 114 |
| 40 | Teofilo Kisanji University(Tabora Centre) | 3 | 10 | 13 |
| 41 | Tumaini University Makumira | 311 | 645 | 956 |
| 42 | Tumaini University Dar es Salaam College | 375 | 290 | 665 |
| 43 | Tumaini University Mbeya Center | 33 | 125 | 158 |
| 44 | Unique Academy Dar es Salaam | 8 | 52 | 60 |
| 45 | United African University of Tanzania | 10 | 49 | 59 |
| 46 | University of Arusha | 142 | 177 | 319 |
| 47 | University of Bagamoyo | 80 | 158 | 238 |
| 48 | University of Iringa | 351 | 553 | 904 |
| 49 | Zanzibar University | 416 | 324 | 740 |
| **Jumla** | | **7,709** | **15,428** | **23,137** |

## Kiambatisho Na.3


## Udahili wa Wanafunzi kwenye vyuo vya Ufundi Stadi - mwaka 2014/15

| Sekta ya Mafunzo | Chini ya Darasa la VII | Darasa la VII | Kidato cha IV | Kidato cha VI na zaidi | Jumla Kuu | % |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Auto Motive | 210 | 16273 | 32633 | 3957 | 53073 | 28% |
| ICT | 9461 | 9441 | 22988 | 3025 | 44915 | 24% |
| Other Trades and Subjects | 2324 | 7559 | 9836 | 1482 | 21201 | 11% |
| Hospitality and Tourism | 178 | 3321 | 15895 | 1055 | 20449 | 11% |
| Business Administration | 1378 | 2078 | 10201 | 835 | 14492 | 8% |
| Electrical | 17 | 1886 | 7863 | 30 | 9796 | 5% |
| Construction | 159 | 4170 | 4210 | 51 | 8590 | 5% |
| Clothing and Textiles | 123 | 5154 | 1774 | 9 | 7060 | 4% |
| Agriculture and Food Processing | 22 | 1144 | 2736 | 54 | 3956 | 2% |
| Mining | 48 | 1211 | 1534 | 517 | 3310 | *2%* |
| Mechanical | 11 | 594 | 1707 | 1 | 2313 | *1%* |
| Printing | | 3 | 280 | | 283 | *0%* |
| Lab Technology | | 44 | 179 | | 223 | *0%* |
| Pedagogy/Andragogy/Training of trainers | | 12 | 14 | | 26 | *0%* |
| **Jumla Kuu** | **13931** | **52890** | **111850** | **11016** | **189687** | ***100%*** |
| ***Asilimia*** | ***7.34%*** | ***27.88%*** | ***58.97%*** | ***5.81%*** | ***100.00%*** | |

## Kiambatisho Na.4: Ongezeko la Udahili kijinsi kwenye Vyuo vya Ufundi Stadi vya Serikali na Binafsi kwa mwaka 2010 - 2014

| Mwaka | Idadi ya Vituo | | | Usajili | | | | | | Jumla ya Usajili | | | Wastani | Asilimia la Ongezeko |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Serikali | | | Binafsi | | | | | | | |
| | Serikali | Binafsi | Jumla | Me | Ke | Jumla | Me | Ke | Jumla | Me | Ke | Jumla | | |
| 2010/11 | 149 | 523 | 672 | 16372 | 6751 | 23123 | 36314 | 45403 | 81717 | 52686 | 52154 | 104840 | | |
| 2011/12 | 164 | 586 | 750 | 23519 | 10072 | 33591 | 40980 | 46777 | 87757 | 64499 | 56849 | 121348 | 16508 | *14%* |
| 2012/13 | 173 | 586 | 759 | 21811 | 15173 | 36984 | 63436 | 45091 | 108527 | 85247 | 60264 | 145511 | 24163 | *17%* |
| 2013/14 | 179 | 670 | 849 | 37986 | 12022 | 50008 | 54849 | 49496 | 104345 | 102559 | 61518 | 164077 | 18566 | *11%* |
| 2014/15 | 189 | 705 | 894 | 44573 | 14650 | 59223 | 64573 | 65891 | 130464 | 109146 | 80541 | 189687 | 25610 | *14%* |
| **Wastani** | **171** | **614** | **785** | **16512** | **5334** | **21846** | **52030** | **50532** | **102562** | **82827** | **62265** | **145093** | **16969** | ***12%*** |

**Kiambatisho Na.5: Chati inayoonesha idadi ya Wanafunzi (kijinsi) waliojiunga na Vyuo Vya Ufundi Stadi mwaka 2010/11 – 2014/15**



Uchambuzi wa udahili katika vyuo vya ufundi stadi vya serikali na vile vya binafsi unaonesha kuwa idadi ya wanafunzi wanaojiunga na vyuo hivi imeongezeka kutoka 104,840 mwaka 2010 hadi 189,687 mwaka 2015; sawa na ongezeko la asilimia 12.

**Kiambatisho Na.6**

**Idadi ya Wanafunzi wenye Mahitaji maalum (kijinsi) waliojiunga na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi na Vyuo vya Mafunzo ya Ufundi Stadi mwaka 2012 – 2014**



| Aina ya Ulemavu | 2012/13 | | Jumla | % | 2013/14 | | Jumla | % | 2014/15 | | Jumla | % |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Me | Ke | | | Me | Ke | | | Me | Ke | | |
| Physical | 53 | 64 | 117 | 44% | 127 | 128 | 255 | 35% | 17 | 16 | 33 | 10% |
| Deaf | 25 | 34 | 59 | 22% | 73 | 260 | 333 | 46% | 50 | 57 | 107 | 33% |
| Mental | 9 | 15 | 24 | 9% | 17 | 21 | 38 | 5% | 101 | 30 | 131 | 40% |
| Albino | 15 | 23 | 38 | 14% | 35 | 35 | 70 | 10% | 11 | 13 | 24 | 7% |
| Multiple | 10 | 10 | 20 | 7% | 0 | 0 | 0 | 0% | 4 | 4 | 8 | 2% |
| Blind | 3 | 0 | 3 | 1% | 5 | 9 | 14 | 2% | 7 | 12 | 19 | 6% |
| Autism | 1 | 1 | 2 | 1% | 2 | 4 | 6 | 1% | 2 | 1 | 3 | 1% |
| Deaf-Blind | 1 | 3 | 4 | 1% | 5 | 5 | 10 | 1% | 2 | 0 | 2 | 1% |
| **Jumla Kuu** | **117** | **150** | **267** | **100%** | **264** | **462** | **726** | **100%** | **194** | **133** | **327** | **100%** |
| **Asilimia** | **44%** | **56%** | **100%** | | **36%** | **64%** | **100%** | | **59%** | **41%** | **100%** | |

**Kiambatisho Na.7**

**Upangaji wa Shule za msingi na Sekondari kwa kiwango cha ufaulu kwa mwaka 2014**

| Mtihani | Mwaka | Kijani | % | Njano | % | Nyekundu | % |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| PSLE | 2015 | 2,022 | 12.562 | 8,603 | 53.448 | 5,471 | 33.99 |
| | 2014 | 913 | 5.7541 | 6,697 | 42.207 | 8,257 | 52.039 |
| | Tofauti | 1,109 | 6.8079 | 1,906 | 11.241 | -2,786 | -18.049 |
| CSEE | 2015 | 325 | 7.0438 | 3,503 | 75.921 | 786 | 17.035 |
| | 2014 | 186 | 4.2206 | 3,732 | 84.683 | 489 | 11.096 |
| | Tofauti | 139 | 2.8232 | -229 | -8.762 | 297 | 5.939 |

## Kiambatisho Na.8

## Mwendo wa Usajili kijinsi kwenye Vyuo vya Ufundi Stadi vya Serikali na Binafsi kwa mwaka 2010 - 2014

| Mwaka | Idadi ya Vituo | | | Usajili | | | | | | Jumla ya Usajili | | | Wastani | *Asilimia la Ongezeko* |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Serikali | | | Binafsi | | | | | | | |
| | Serikali | Binafsi | Jumla | Me | Ke | Jumla | Me | Ke | Jumla | Me | Ke | Jumla | | |
| 2010/11 | 149 | 523 | 672 | 16372 | 6751 | 23123 | 36314 | 45403 | 81717 | 52686 | 52154 | 104840 | | |
| 2011/12 | 164 | 586 | 750 | 23519 | 10072 | 33591 | 40980 | 46777 | 87757 | 64499 | 56849 | 121348 | 16508 | *14%* |
| 2012/13 | 173 | 586 | 759 | 21811 | 15173 | 36984 | 63436 | 45091 | 108527 | 85247 | 60264 | 145511 | 24163 | *17%* |
| 2013/14 | 179 | 670 | 849 | 37986 | 12022 | 50008 | 54849 | 49496 | 104345 | 102559 | 61518 | 164077 | 18566 | *11%* |
| 2014/15 | 189 | 705 | 894 | 44573 | 14650 | 59223 | 64573 | 65891 | 130464 | 109146 | 80541 | 189687 | 25610 | *14%* |
| **Wastani** | **171** | **614** | **785** | **16512** | **5334** | **21846** | **52030** | **50532** | **102562** | **82827** | **62265** | **145093** | **16969** | ***12%*** |